NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU

28 Novemba 2023

Kwa Wabahá 'í wa Ulimwengu

Marafiki wapendwa Sana,

Mnamo 27 Novemba 2021, katikati ya usiku mtulivu, wenye giza, takribani wawakilishi mia sita wa Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa na Halmashauri za Kibahá'í za Kanda walikusanyika, pamoja na wajumbe wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa, hali kadhalika na wafanyakazi wa Makao Makuu ya Kibahá'i ya Ulimwengu, kuadhimisha kwa heshima na taadhima, katika viunga vya Kaburi Lake Takatifu, miaka mia moja ya kufariki kwa ‘Abdu‘l-Bahá. Usiku ule wote, kwa mzunguko wa dunia, jamuiya za Kibahá'í kote ulimwenguni pia zilikusanyika kwa umakinifu wenye moyo wa ibada, katika ujirani na vijiji, miji na majiji, kutoa heshima kuu kwa Mtu huyo asiye na mfano katika historia ya kidini, na katika kutafakari kwa kina juu ya karne ya mafanikio ambayo Yeye Mwenyewe alikuwa ameyaanzisha.

Jumuiya hii‒watu wa Bahá’, wapenzi wenye shauku wa ‘Abdu’l-Bahá—sasa mamilioni ya watu wenye nguvu, leo imeenea katika maeneo takribani laki moja katika nchi na maeneo 235. Imeibuka kutoka kwenye giza na kutwaa nafasi yake kwenye jukwaa la ulimwengu. Imeinua mtandao wa maelfu ya asasi, kutoka ngazi ya chini hadi ngazi ya kimataifa, ikiunganisha anuwai ya watu katika kusudi la pamoja la kutoa sura kwa mafundisho ya Bahá’u’lláh kwa ajili ya mabadiliko ya kiroho na maendeleo ya kijamii. Katika kanda nyingi, mtindo wake wa kujenga jumuiya hai za mahali umekumbatia maelfu—na katika baadhi, makumi ya maelfu—ya roho. Katika mazingira kama haya, njia mpya ya maisha inapata umbo, ikijipambanua kwa tabia yake ya kiibada; kujitolea kwa vijana kwa ajili ya elimu na huduma; mazungumzo yenye dhamira miongoni mwa familia, marafiki, na jamaa juu ya mada zenye umuhimu wa kiroho na kijamii; na jitihada za pamoja za maendeleo ya kimwili na kijamii. Maandiko Matakatifu ya Imani yametafsiriwa katika lugha zaidi ya mia nane. Uinuaji wa Mashriqu’l-Adhkár za kitaifa na za mahali hutangulia utokeaji wa maelfu ya vituo vya siku zijazo vilivyokusudiwa kwa ajili ya ibada na huduma. Makao Makuu ya Kiroho na Kiutawala ya Imani ya Ulimwengu yameanzishwa katika miji pacha mitakatifu ya ‘Akká na Haifa. Na licha ya mapungufu ya sasa ya jumuiya, yaliyo wazi kabisa yanapotazamwa kuhusiana na maadili yake na matamanio yake ya juu—hali kadhalika na umbali unaoitenganisha kutoka ufikiaji wa lengo lake la mwisho, utambuzi wa umoja wa jamii ya binadamu—raslimali zake, uwezo wake wa kiasasi, uwezo wake wa kudumisha ukuaji wa kiutaratibu na maendeleo, ushiriki wake na asasi zenye mtazamo sawa, na kujihusisha kwake katika, na ushawishi chanya kwa jamii husimama kwenye kilele cha juu kisicho na mfano cha mafanikio ya kihistoria.

Imani imefika mbali kiasi gani tangu wakati huo, karne moja iliyopita, wakati ‘Abdu’l-Bahá alipoondoka katika ulimwengu huu! Alfajiri ya siku ile ya huzuni, habari za kufariki Kwake zilienea katika jiji zima la Haifa, zikiiteketeza mioyo kwa majonzi. Maelfu walikusanyika kwa ajili ya mazishi Yake: wadogo kwa wakubwa, wenye hadhi ya juu kwa wenye hadhi ya chini, maafisa maarufu wa serikali na wa umma—Wayahudi kwa Waislam, Wadruzi kwa Wakristo, hali kadhalika Wabahái— mkusanyiko ambao mfano wake jiji hilo halikupata kushuhudia. Machoni pa ulimwengu, ‘Abdu’l-Bahá alikuwa mshindi wa amani ya ulimwengu na umoja wa jamii ya

binadamu, mtetezi wa wanyonge na mkuzaji wa haki. Kwa watu wote wa ‘Akká na Haifa, Yeye alikuwa baba mwenye upendo na Rafiki, mshauri mwenye hekima na kimbilio kwa wote wenye uhitaji. Kwenye mazishi Yake walionesha hisia za ari ya juu ya upendo na maombolezo.

Kwa kawaida, hata hivyo, ni Wabahá'í ndio waliojihisi hasa kutokuwepo Kwake. Yeye alikuwa zawadi yenye thamani kubwa iliyotolewa na Mdhihitrishaji wa Mungu ili kuwaongoza na kuwalinda, Kitovu na Mhimili wa Agano lisilo na kifani na likunjukalo la Bahá 'u' lláh, Mfano kamili wa mafundisho Yake, Mfasiri asiyekosea wa Neno Lake, mfano halisi wa kila maadili bora ya Kibahá’i. Katika kipindi chote cha maisha Yake, ‘Abdu‘l-Bahá alifanyakazi bila kuchoka katika kumtumikia Bahá'u'lláh, akitimiza, kikamilifu, wajibu mtakatifu wa Baba Yake. Aliilea kwa uaminifu na kuilinda mbegu yenye thamani ambayo ilikuwa imepandwa. Aliilinda Hoja tangu mwanzo wa kuzaliwa kwake na, akiongoza ueneaji wake huko Magharibi, huko alianzisha chimbuko la utawala wake. Aliimarisha nyayo za waumini na kuinua kundi la mashujaa na watakatifu. Kwa mikono Yake Mwenyewe, aliyazika mabaki matakatifu ya Báb katika katika kaburi kubwa, zuri aliloijenga kwenye Mlima Carmel, akitunza kwa dhati Makaburi pacha Matakatifu, na na kuweka misingi ya makao makuu ya kiutawala ya Imani ya ulimwengu. Aliikinga Imani kutoka kwa maadui wake waliokiri waziwazi, wa ndani na nje. Alilinda Imani dhidi ya maadui zake waliokiri wazi wazii, wa ndani na nje. Alifunua Mkataba wa thamani wa kushiriki mafundisho ya Bahá'u'lláh na watu kote ulimwenguni, hali kadhalika Mkataba ambao uliweka na kuanzisha michakato ya Utaratibu wa Kiutawala. Maisha Yake yalidumu katika kipindi chote cha Zama za Kishujaa zilizozinduliwa kwa tangazo la Báb; kupaa kwake kuliikaribisha Zama mpya ambazo sura zake bado zilikuwa hazijulikani kwa waumini.  Je, ni kitu gani kingewapata wapendwa wake? Bila Yeye, bila mwongozo Wake endelevu, wakati ujao ulionekana kutokuwa na uhakika na usio na matumaini.

Akiwa amehuzunishwa na taarifa za kufariki kwa ‘Abdu’l-Bahá, mjukuu Wake wa kiume, Shoghi Effendi aliharakisha kutoka kwenye masomo yake huko nchini Uingereza kuelekea Nchi Takatifu, ambako alipata pigo la pili la kushtua. ‘Abdu‘l-Bahá alikuwa amemteua yeye kuwa Mlinzi na Mkuu wa Imani, akiukabidhi ulimwengu wa Kibahá 'i chini ya uangalizi wake. Kwa majonzi na uchungu, lakini lakini akiimarishwa na msaada usioshindwa wa mpendwa binti wa Bahá'u'lláh, Bahíyyih Khánum, Shoghi Effendi alivaa joho zito la ofisi yake na akaanza kutathmini hali na matarajio jumuiya changa.

Tangazo la uteuzi wa Shoghi Effendi kuwa Mlinzi lilipokelewa kwa faraja, shukrani, na viapo vya uaminifu na kundi la waumini. Uchungu wa kutengana kwao na Bwana ulitulizwa na uhakikisho katika Agano na Wasia kwamba Yeye hakuwa Amewaacha peke yao. Wachache wasio waaminifu, hata hivyo, walimpinga mrithi mteule wa Abdu’l-Bahá na, wakichochewa na matamanio yao wenyewe na ubinafsi, waliinuka dhidi yake. Usaliti wao katika kipindi kile muhimu cha mpito ulichagizwa na hila mpya za wapinzani waliokiri wazi wazi wa Bwana. Ingawa akiwa bado amekandamizwa sana kwa maumivu ya moyo na majaribu kama hayo, na mbele ya vizuizi vingine vya kuogofya, Shoghi Effendi alianza kuwaandaa waumini wa jumuiya za Kibaha'i zilizosambaa kwa mapana kuanza kazi kabambe ya kuweka misingi ya Utaratibu wa Kiutawala. Watu ambao hapo awali walichochewa na haiba ya kipekee ya ‘Abdu' l- Bahá pole pole walianza kuratibu juhudi zao katika shughuli ya pamoja chini ya uongozi wenye uvumilivu lakini thabiti wa Mlinzi.

Wakati Wabahá'í walipoanza kuyakabili majukumu yao mapya, Shoghi Effendi alifurahia jinsi ufahamu wao wa mwanzo ulivyokuwa, hadi sasa, wa ufunuo Mtakatifu ulio katika milki yao na jinsi changamoto zilizo mbele yao zilivyokuwa za kutisha. “Ni mpana jinsi gani Ufunuo wa Bahá'u'lláh! Ni kwa wingi jinsi gani ukuu wa baraka Zake zilizomiminwa juu ya jamii ya wanadamu katika siku hii!” yeye aliandika: “Na bado, ni duni, jinsi gani, ni finyu jinsi gani ufahamu wetu wa umuhimu na utukufu wao! Kizazi hiki kipo karibu mno na Ufunuo wenye nguvu kubwa kiasii hicho kutambua, kwa kiwango chake kamili, uwezekano usio na kikomo wa Imani Yake, sifa isiyo na mfano ya Hoja Yake, na vipindi vitakatifu vya ajabu vya Majaliwa Yake." "Maudhui ya Wasia wa Bwana ni mengi mno kwa kizazi cha sasa kuyaelewa", katibu wake aliandika kwa niaba yake. “Inahitaji angalau karne moja ya utendaji hasa kabla hazina za hekima zilizofichwa ndani mwake kuweza kufichuliwa.” Ili kuelewa asili na ukubwa wa muono wa Bahá'u'lláh wa Utaratibu mpya wa Ulimwengu, yeye alielezea, "Lazima tuamini kwenye wakati, na mwongozo wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu ya Mungu, kujipatia uekewa dhahiri na mkamilifu wa maagizo na athari zake."

Wakati huu, kufuatia, kama ufanyavyo, kukamilika kwa karne nzima ya "utendaji kazi halisi", hutoa mahali pafaapo pa neema ambapo kutoka hapo umaizi mpya hukusanywa. Na kwa hivyo tumechagua fursa ya maadhimisho haya kusita kidogo ili kutafakari pamoja nanyi juu ya hekima iliyomo katika maagizo ya Wasia na Agano, kufuatilia mwelekeo wa ukunjukaji wa Imani na kuona mwambatano wa hatua za maendeleo yake ya kimfumo, kutambua fursa zilizopo katika michakato inayoendesha maendeleo yake, na kuthamini ahadi yake kwa miongo ijayo kadiri nguvu yake ya kuunda upya jamii inavyozidi kudhihirishwa ulimwenguni kupitia athari iongezekayo ya Ufunuo wa ajabu wa Bahá 'u' lláh.

Kutafsiri kile kilichoandikwa katika uhalisia na vitendo

Kusudi la Bahá'u'lláh ni kuanzisha hatua mpya katika maendeleo ya binadamu—umoja wa kiasili na wa kiroho wa watu na mataifa ya ulimwengu—hivyo kuashiria kuja kwa zama za mbari ya wanadamu na kupambanuliwa, katika utimilifu wa wakati, kwa uibukaji wa ustaarabu na utamaduni wa ulimwengu. Kwa kusudi hili, Yeye alifunua mafundisho Yake kwa ajili ya mabadiliko ya ndani na ya nje ya maisha ya mwanadamu. "Kila mstari ambao Kalamu hii imeufunua ni lango angavu na ling'aalo ambalo hufunua utukufu wa maisha matakatifu na ya ucha-Mungu, ya matendo safi na yasiyo na mawaa", Yeye alieleza. Na katika Nyaraka zisizohesabika Yeye, Tabibu Mtakatifu, alibaini magonjwa yanayowatesa wanadamu na kuweka wazi tiba Yake iponyayo kwa ajili ya "uinuliwaji, maendeleo, elimu, ulinzi na kuzaliwa upya kwa watu wa ulimwengu.” Bahá'u'lláh alielezea kwamba "Miito na ujumbe Tulioutoa kamwe haukukusudiwa kuifikia au kuinufaisha nchi moja au aina moja tu ya watu." "Inampasa kila mtu mwenye umaizi na uelewa", Yeye aliandika, "ajitahidi kutafsiri kile kilichoandikwa katika ukweli na vitendo….Amebarikiwa na ni mwenye furaha yule ambaye huinuka kuendeleza raghba bora kabisa za watu na koo za dunia."

Kazi ya kujenga ulimwengu uliokomaa, wenye amani, haki, na umoja ni jukumu kubwa ambalo watu na mataifa yote lazima yaweze kushiriki. Jumuiya ya Kibahá'í inawakaribisha wote kujiunga katika juhudi hii kama wahusika wakuu katika shughuli ya kiroho ambayo inaweza kuzishinda nguvu za uchangukaji zinazouharibu utaratibu wa zamani wa kijamii na kutoa muundo dhahiri kwenye mchakato jumuishi ambao utasababisha ukunjukaji wa utaratibu mpya badala yake. Zama za Ujenzi ni kile kipindi muhimu katika maendeleo ya Imani ambacho marafiki wanazidi kuthamini ujumbe ambao Bahá 'u' lláh amewakabidhi, kuimarisha uelewa wao wa athari na matokeo ya Neno Lake lililofunuliwa, na kwa utaratibu kukuza uwezo wao wenyewe na ule wa wengine—ili wayaweke katika vitendo mafundisho Yake kwa ajili ya uboreshaji wa ulimwengu.

Tangu mwanzo wa utumishi wake, Shoghi Effendi aliwaongoza Wabahá 'í katika jitihada zao za kupata uelewa wa kina wa wito wao, ambao ungeelezea wazi utambulisho na kusudi lao. Yeye aliwafafanulia kwa kina maana ya kuja kwa Bahá 'u' lláh, muono Wake kwa jamii ya wanadamu, historia ya Hoja, michakato ya kujenga upya jamii, na nafasi ambayo Wabahá'í lazima wachukue katika kuchangia maendeleo ya wanadamu. Alielezea kwa muhtasari asili ya maendeleo ya jumuiya ya Kibahá'í ili marafiki watambue kwamba ingepitia mabadiliko mengi, mara nyingi yasiyotarajiwa, kwa zaidi ya miongo na karne. Pia alielezea lahaja ya hali ya hatari na ushindi, akiwaandaa kwa ajili ya njia vizingo vingi ambayo lazima waipitie. Alitoa wito kwa Wabahá'í kuboresha tabia zao na kunoa akili zao ili kukabiliana na changamoto za kuujenga ulimwengu mpya. Aliwasihi wasikate tamaa pale watakapokumbana na matatizo ya jumuiya changa na inayoendelea kukua kwa kasi au ufukara na kuzorota mazingira ya zama za ghasia, akiwakumbusha kwamba udhihirisho kamili wa ahadi za Bahá 'u' lláh upo katika siku zijazo. Alielezea kwamba Wabahá 'í walipaswa wawe chachu—ushawishi upenyezao na uhuishao—ambao ungeweza kuwahamasisha wengine kuinuuka na kuishinda mitindo iliyoimarishwa ya mgawanyiko, migogoro, na kushindania madaraka, ili matamanio ya juu ya jamii ya binadamu hatimaye yaweze kufikiwa.

Wakati wa kuimarisha maeneo haya mapana ya uelewa, Mlinzi pia aliwaongoza waumini, hatua kwa hatua, kujifunza jinsi ya kuanzisha kwa ufanisi msingi wa kimuundo wa Utaratibu wa Utawala na kushiriki kimpangilio mafundisho ya Bahá'u'lláh na wengine. Kwa ustahimilivu alielekeza juhudi zao kwa kufafanua pole pole asili, kanuni, na taratibu ambazo zinaonesha Utaratibu huo, huku akiinua uwezo wao wa kufundisha Imani, wa mtu binafsi na wa pamoja. Juu ya kila jambo muhimu, angetoa mwelekeo na waumini wangeshauriana na kujitahidi kutumia mwongozo wake, wakishiriki tajiriba yao naye na kuibua maswali walipokabiliwa na shida za kutatanisha. Kisha, kwa kuzingatia tajiriba inayokusanya, Mlinzii atatoa mwongozo wa ziada na kufafanua dhana na kanuni ambazo zitawawezesha marafiki kurekebisha hatua zao kama inavyohitajika, hadi juhudi zao zitakapoonekana kuwa na ufanisi na zingeweza kutumika kwa mapana zaidi. Katika kuitikia mwongozo wake, marafiki walionesha imani isiyoyumba katika ukweli wa Neno lililofunuliwa, imani isiyoyumba katika maono yake na hekima isiyo na makosa, na azimio lisiloyumba la kubadilisha vipengele mbalimbali vya maisha yao kulingana na muundo uliowekwa katika Mafundisho. Kwa namna hii, uwezo wa kujifunza jinsi ya kutumia Mafundisho ulikuzwa hatua kwa hatua ndani ya jumuiya. Ufanisi wa mbinu hii ulioneshwa wazi zaidi wakati wa kilele cha htumishi wake, wakati ulimwengu wa Kibahá 'í ulipounganisha nguvu zake kwa ajili ya mafanikio yasiyo na kifani ya Mapambano ya Kiroho ya Miaka Kumi.

Jitihada za Shoghi Effendi kuwaweka waumini kwenye njia ya ujifunzaji ziliongezwa zaidi, baada ya kufariki kwake, chini ya uongozi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Hadi kufikia miaka ya mwishoni ya karne ya kwanza ya Zama za Ujengii, vipengele muhimu vya mchakato wa ujifunzaji ambavyo vilikuwa katika hali changa mwanzoni mwa karne hiyo vilieleweka kwa makusudi na kutekelezwa kwa mpangilio na Wabahá'í kote ulimwenguni kwa juhudi zao zote.

Leo jumuiya ya Kibahá'í inapambanuliwa kwa mtindo wa utendaji unaoainishwa kwa ujifunzaji, ushauriano, utendaji na tafakari. Inazidi kuongeza kwa kasi uwezo wake wa kutumia Mafundisho katika nafasi mbalimbali za kijamii na kushirikiana na wale walio katika jamii pana zaidi ambao hushiriki shauku ya kuhuisha misingi ya kimwili na ya kiroho ya utaratibu wa kijamii. Katika chombo cha mabadiliko cha nafasi hizi, kwa kadri iwezekanavyo, watu binafsi na jumuiya huwa wahusika wakuu wa maendeleo yao wenyewe, kukumbatia umoja wa ubinadamu huondoa ubaguzi na utofauti, mwelekeo wa kiroho wa maisha ya mwanadamu unakuzwa kupitia kufuata kanuni na kuimarisha tabia ya ibada ya jamii, na uwezo wa kujifunza unakuzwa na kuelekezwa kwenye mabadiliko ya kibinafsi na ya kijamii. Jitihada za kuelewa maana ya kile ambacho Bahá 'u'lláh amekifunua na kutumia tiba Yake iponyayo sasa zimekuwa wazi zaidi, za makusudi zaidi, na sehemu isiyofutika ya utamaduni wa Kibahá'í. Uelewa wa mchakato wa ujifunzaji na upanuzi wake kote ulimwenguni, kuanzia ngazi ya chini hadi uga wa kimataifa, ni miongoni mwa matunda bora kabisa ya karne ya kwanza ya Zama za Ujenzi. Mchakato huu utazidi kuarifu kazi ya kila asasi, jumuiya, na mtu binafsi katika miaka ijayo, kadiri ulimwengu wa Kibahá'í daima unavyochukua changamoto kubwa zaidi na daima kutolewa katika hatua kubwa zaidi za nguvu ya Imani ya ujenzi wa jamii.

Katika juhudi zake za kuwasaidia marafiki kwenye uelewa wao wa maendeleo ya Imani na wajibu wao husika, Shoghi Effendi alirejelea, “msukumo wa mara tatu unaotokana na ufunuo wa Waraka wa Carmel na Bahá'u'lláh na Wasia na Agano pamoja na Nyaraka za Mpango Mtakatifu zilizorithishwa na Kitovu cha Agano Lake—Mikataba mitatu ambayo imeanzisha michakato mitatu tofauti, wa kwanza unaofanya kazi katika Nchi Takatifu kwa ajili ya maendeleo ya asasi za Imani kwenye Makao yake ya Ulimwengu na mingine miwili, katika ulimwengu wote wa Kibahá'í, kwa ajili ya uenezaji wake na uanzishwaji wa Utaratibu wake wa Kiutawala". Michakato inayohusiana na kila moja ya Mikataba hii Mitakatifu inategemeana na inaimarishana. Utaratibu wa Kiutawala ni chombo kikuu cha muendelezo wa Mpango Mtakatifu, ambapo Mpango ni wakala wenye nguvu kabisa kwa ajili ya maendeleo ya muundo wa kiutawala wa Imani. Maendeleo katika Makao Makuu ya Ulimwengu, kiini cha moyo na mishipa ya utawala, hutoa ushawishi mkubwa juu ya shirika la jumuiya ya kimataifa na kwa upande wake huathiriwa na nguvu zake. Ulimwengu wa Kibahá'í hubadilika kila wakati na hukua taratibu na kiasili kama watu binafsi, jumuiya na asasi zikijitahidi kutafsiri katika uhalisia kweli za Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Sasa, mwishoni mwa karne ya kwanza ya Zama za Ujenzi, ulimwengu wa Kibahá'í unaweza kuelewa kwa ukamilifu zaidi athari za kiasili zilizomo katika Mikataba hii ya milele kwa ajili ya maendeleo ya Imani. Na kwa sababu umeongeza uelewa wake wa mchakato ambamo unashiriki, unaweza kutambua vizuri zaidi tajiriba yake katika karne iliyopita na unaweza kutenda kwa ufanisi zaidi ili kufanikisha madhumuni yaliyokusudiwa ya Bahá'u'lláh kwa jamii ya binadamu katika miongo na karne zijazo.

## Udumishaji wa Agano

Ili kulinda umoja wa Imani Yake, kudumisha uadilifu na unyumbulifu wa mafundisho Yake, na kuhakikisha maendeleo ya wanadamu wote, Bahá'u'lláh alianzisha Agano na wafuasi Wake ambalo ni la kipekee katika kumbukumbu za historia ya kidini kwa mamlaka yake na asili yake ya wazi na ya kina. Katika Kitabu Chake Kitakatifu Kabisa na katika Kitabu cha Agano Lake, hali kadhalika katika Nyaraka zingine, Bahá'u'lláh aliagiza kwamba baada ya kufariki Kwake marafiki waMgeukie Abdu'l-Bahá, Kitovu cha Agano, kuongoza masuala ya Imani. Katika Wasia na Agano Lake, 'Abdu'l-Bahá aliliendeleza Agano kwa kuweka maagizo kwa ajili ya Utaratibu wa Kiutawala ulioamriwa katika Maandiko ya Bahá'u'lláh, hivyo, kuhakikisha uendelezaji wa mamlaka na uongozi kupitia asasi pacha za Ulinzi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, hali kadhalika uhusiano imara baina ya watu binafsi na asasi ndani ya Imani.

Historia imeonesha kabisa kwamba dini inaweza kutumika ama kama chombo chenye nguvu cha ushirikiano cha kusukuma maendeleo ya ustaarabu, au kama chanzo cha migogoro ambayo husababisha madhara yasiyohesabika. Nguvu ya dini iunganishayo na istaarabishayo huanza kupungua pale wafuasi wanapokosa kukubaliana juu ya maana na matumizi ya mafundisho matakatifu, na jumuiya ya waaminifu hatimaye hugawanyika katika makundi na madhehebu yashindanayo. Kusudi la Ufunuo wa Bahá'u'lláh ni kuanzisha umoja wa binadamu na kuwaunganisha watu wote, na hatua hii ya mwisho na ya juu kabisa katika mageuzi ya jamii haiwezi kufikiwa ikiwa Imani ya Kibahá'i itaangukia kwenye maradhi ya kugawanyika katika madhehebu na kuzimuliwa kwa Ujumbe mtakatifu ulioshuhudiwa hapo zamani. Ikiwa Wabahá'i "hawawezi kuungana katika jambo moja", Abdu'l-Bahá huona, "watawezaje kuleta umoja wa binadamu?" Na Yeye huthibitisha: "Leo mamlaka yenye nguvu ya ulimwengu wa uwepo ni nguvu ya Agano ambayo kama vile ateri inavyopuma katika mwili wa ulimwengu wa nasibu na huulinda umoja wa Kibahá'í."

Ya kwanza kabisa miongoni mwa mafanikio ya karne iliyopita ni ushindi wa Agano, ambalo lililinda Imani kutokana na mgawanyiko na kuisukuma kukumbatia na kuchangia kwenye uwezeshaji wa watu na mataifa yote. Swali lipenyezalo la Bahá'u'lláh ambalo limo kwenye kiini cha dini– "Wewe utafunga wapi kamba ya imani yako na kukaza kifungo cha utiifu wako?"— huchukua umuhimu mpya na wa lazima kwa wale wanaomtambua Yeye kama Mdhihirishaji wa Mungu kwa Siku hii. Ni mwito wa uthabiti katika Agano. Mwitikio wa jjumuiya ya Kibahá'í umekuwa ufuasi thabiti kwa maagizo ya'Wasia na Agano la Abdu'l-Bahá. Tofauti na mahusiano ya nguvu za kiulimwengu ambamo chombo chenye mamlaka hulazimisha utiifu, uhusiano kati ya Mdhihirishaji wa Mungu na waumini, na kati ya mamlaka iliyoteuliwa ya Agano na jumuiya, unaongozwa na ujuzi fahamivu na upendo. Katika kumtambua Bahá'u'lláh, muumini huingia kwa hiari katika Agano Lake kama kitendo cha dhamiri huru na, kutokana na upendo Kwake, hubakia imara katika kuzingatia mahitaji yake. Kwenye kuhitimisha karne ya kwanza ya Zama za Ujenzi, Ulimwengu wa Kibahá'i umefikia kuelewa kwa ukamilifu zaidi na kutenda kufuatana na maagizo ya Agano la Bahá'u'lláh, na seti ya kipekee ya uhusiano imeanzishwa miongoni mwa waumini ambayo huunganisha na kuelekeza nguvu zao katika kutekeleza ujumbe wao mtakatifu. Mafanikio haya, kama mengine mengi, yalikuwa ni matunda ya migogoro waliyoishinda.

Uwepo wa Agano haumaanishi kwamba hakuna mtu atakayejaribu kamwe kuigawa Imani, kuidhuru, au kudumaza maendeleo yake. Lakini inahakikisha kwamba kila jaribio kama hilo limekusudiwa kushindwa. Kufuatia kifo cha Bahá'u'lláh, baadhi ya watu wenye tamaa ya makuu, wakiwemo kaka zake Abdu'l-Bahá, walijaribu kunyakua mamlaka aliyopewa Abdu'l-Bahá na Bahá'u'lláh na walipanda mbegu za mashaka ndani ya jumuiya, wakijaribu na wakati mwingine kuwapotosha wale wenye kusitasita. Shoghi Effendi, wakati wa utumishi wake, hakushambuliwa tu na wale waliokuwa wamevunja Agano na kumpinga Abdu'l-Bahá, bali pia na wengine ndani ya jumuiya waliokataa kutambua uhalali wa Utaratibu wa Utawala na kuhoji mamlaka ya Ulinzi. Miaka kadhaa baadaye, Shoghi Effendi alipofariki, shambulio jipya juu ya Agano liliibuka pale mtu mmoja aliyepotoshwa mno, licha ya kuhudumu kwa muda mrefu kama Mkono wa Hoja ya Mungu, alipofanya jaribio lisilo na msingi na lisilo na maana kudai kuwa Mlinzi yeye mwenyewe, licha ya maagizo dhahiri yaliyowekwa katika Wasia na Agano. Baada ya uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, pia ilikuja kuwa ndiyo shabaha ya wapinzani madhubuti wa Hoja. Miongo kadhaa ya hivi karibuni, wachache kutoka ndani ya jumuiya, wakijinadi wenyewe kama wenye ujuzi zaidi kuliko wengine, bila mafanikio walitafuta kufasiri upya mafundisho ya Kibahá'í yahusuyo maagizo ya Agano ili kutilia shaka juu ya mamlaka ya Nyumba ya Haki na kudai haki fulani, kwa kutokuwepo kwa Mlinzi aliye hai, ambayo ingewawezesha kuendesha masuala ya Imani kwa namna wachaguavyo wao wenyewe.

Kwa zaidi ya karne moja, basi, Agano lililoanzishwa na Bahá'u'lláh na kuendelezwa na Abdu'l-Bahá lilishambuliwa kwa njia mbalimbali na wapinzani wa ndani na nje, lakini hatimaye halikufanikiwa. Ambapo, kila kipindi, watu wengine walipotoshwa au kupoteza imani, mashambulio yalishindwa kugeuza au kuifafanua upya Hoja au kutengeneza ufa wa kudumu katika jumuiya. Katika kila kisa, kugeukia kwenye kitovu kilichoteuliwa cha mamlaka cha wakati huo— 'Abdu'l-Bahá, Mlinzi, au Nyumba ya Haki ya Ulimwengu—maswali yalijibiwa na matatizo kutatuliwa. Kadiri kundi zima la waumini lilivyokuwa katika uelewa wake wa, na uthabiti katika Agano, lilijifunza kutokubaliana na aina za mashambulio na na uwasilishaji potofu ambao, katika enzi za awali, yalitishia uwepo na kusudi lenyewe la Imani. Uadilifu wa Hoja ya Bahá'u'lláh daima hubakia salama.

Kila kizazi cha Wabahá'i, hata mtazamo wao wa kiroho uwe mkubwa jinsi gani, bila shaka kitakuwa na ufahamu wenye mipaka wa athari kamili za mafundisho ya Bahá'u'lláh, kutokana na mapungufu ya mazingira yao wenyewe ya kihistoria na hatua mahsusi ya ukuaji wa kiasili wa Imani. Katika Zama za Ushujaa za Imani, kwa mfano, waumini walilazimika kupitia kile ambacho kwa hakika walikuwa na tajiriba nacho muda fulani kama mfululizo wa mabadiliko ya kutatanisha na ya kimapinduzi kutoka Kipindi Kitakatifu cha Báb hadi kile cha Bahá'u'lláh, na kisha kwenye utumishi wa Abdu'l-Bahá—ambayo yote, kwa mtazamo wa hapo awali na ufafanuzi uliotolewa na Shoghi Effendi, sasa yanaeleweka kwa urahisi kama vitendo vinavyofuatana katika tamthilia takatifu inayokunjuka. Vivyo hivyo, leo, baada ya kazi zisizochoka za jumuiya kwa karne nzima, ya kwanza ya Zama za Ujenzi, inawezekana kuelewa zaidi umuhimu, kusudi, na kutodhurika kwa Agano—ule urithi usiokadirika wa Bahá'u'lláh kwa wafuasi Wake. Uelewa wa shida wa asili ya

Agano na uthabiti ambao ufahamu kama huo huleta na kudumisha utaendelea kuwa wa lazima kwa umoja na maendeleo katika Kipindi hiki Kitakatifu.

Sasa ni dhahiri na imethibitishwa kwa uthabiti kwamba Agano la Bahá'u'lláh hutoa vitovu viwili vya mamlaka. Cha kwanza ni Kitabu: Ufunuo wa Bahá'u'lláh, pamoja na maandishi ya `Abdu'l-Bahá na Shoghi Effendi yanayounda fasiri yenye mamlaka na ufafanuzi wa Neno la Kiuumbaji. Kwa kufariki kwa Shoghi Effendi, zaidi ya karne moja ya mwendelezo wa kitovu hicho chenye mamlaka kilifikia mwisho. Hata hivyo, uwepo wa Kitabu unahakikisha kwamba Ufunuo usioghoshiwa na fasiri potofu au fafanuzi za kibinadamu unapatikana kwa kila muumini, kwa kweli kwa wanadamu wote.

Kitovu cha pili cha mamlaka ni Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, ambayo, kama Maandiko Matakatifu yanavyothibitisha, ipo chini ya uangalizi na mwongozo usiokosea wa Bahá'u'lláh na Báb. `"Hebu tusidhani kwamba Nyumba ya Haki itachukua uamuzi wowote kulingana na dhana na maoni yake yenyewe", Abdu'l-Bahá anaeleza. "Mungu apishie mbali! Nyumba Kuu ya Haki itachukua maamuzi na kuanzisha sheria kupitia uvuvio na uthibitisho wa Roho Mtakatifu, kwani ipo katika uhifadhi na chini ya kimbilio na ulinzi wa Uzuri Uliobarikiwa". "Mungu kwa kweli atawawavuvia kwa chochote Anachokitaka," Bahá'u'lláh anatangaza. "Wao, na si kundi la wale ambao, huwachagua, ama moja kwa moja au kwa njia isiyo ya moja kwa moja," Shoghi Effendi anasema, "kwa hivyo wamefanywa wapokeaji wa mwongozo mtakatifu ambao wakati huo huo ndio damu ya uhai na kinga ya mwisho ya Ufunuo huu."

Mamlaka na wajibu ambao kwao Nyumba ya Haki imetwishwa hujumuisha yote yanayohitajika kwa ajili ya kuhakikisha utimilifu wa kusudi la Bahá'u'lláh kwa wanadamu. Kwa zaidi ya nusu karne, Ulimwengu wa Kibahá'í umeshuhudia moja kwa moja upeo na maonesho yao, ikiwa ni pamoja na kutangazwa kwa Sheria ya Mungu, uhifadhi na usambazaji wa Maandiko Matakatifu ya Kibahá'í, kuinua kwa Utaratibu wa Kiutawala na kuundwa kwa asasi mpya, kupanga hatua zinazofuatana katika ukunjukaji wa Mpango wa Mungu, na ulinzi wa Imani na uhifadhi wa umoja wake, pamoja na jitihada zinazowezesha kutunza heshima ya kibinadamu, maendeleo ya ulimwengu, na mwangaza wa watu wake. Ufafanuzi wa Nyumba ya Haki hutatua matatizo yote magumu, maswali yasiyoeleweka, matatizo ambayo yamesababisha tofauti, na masuala ambayo hayajaandikwa kwa uwazi katika Kitabu. Nyumba ya Haki itatoa mwongozo kwa Kipindi chote Kitakatifu kulingana na mahitaji ya wakati, na hivyo kuhakikisha kwamba Hoja, kama vile kiumbe hai, huweza kukabiliana na mahitaji na masharti ya jamii inayoendelea kubadilika daima. Na inahakikisha kwamba hakuna awezaye kubadilisha asili ya ujumbe wa Bahá'u'lláh au sifa muhimu za Hoja.

Katika Kitáb-i-Íqán (Kitabu cha Yakini), Bahá'u'llah anauliza, "Ni 'ukandamizaji' gani mbaya zaidi kuliko kwamba roho inayotafuta ukweli, na inayotamani kufikia ujuzi wa Mungu, isijue ni wapi pa kwenda kuupata na kutoka kwa nani ikautafuta?" Ulimwengu unaopuuza kwa kiasi kikubwa nuru ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh, unajikuta ukigawanyika na kuchanganyikiwa juu ya masuala ya ukweli, maadili, utambulisho, na kusudi, na kutatanishwa na athari inayoongeza kasi na kuharibika kwa nguvu za utenganishaji. Kwa jumuiya ya Kibahá'í, walakini, Agano hutoa chanzo cha uwazi na kimbilio, cha uhuru na nguvu. Kila muumini yupo huru kuchunguza bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh, kufikia hitimisho binafsi, kushiriki uelewa kwa unyenyekevu na

wengine, na kujitahidi kutumia Mafundisho siku hadi siku. Jitihada za pamoja zinaunganishwa na umakinikiaji kupitia mashauriano na mwongozo wa asasi, zikibadilisha uhusiano baina ya watu binafsi, ndani ya familia, na baina ya jumuiya, na kukuza maendeleo ya kijamii.

Kutokana na upendo kwa Bahá'u'lláh na kuhakikishiwa na maagizo Yake ya wazi, watu binafsi, jumuiya, na asasi hupata katika vitovu hivyo viwili vya mamlaka vya Agano miongozo ihitajikayo kwa ajili ya ukunjukaji wa Imani na kuhifadhi uadilifu wa Mafundisho. Kwa namna hii, Agano linalinda ma kuhifadhi mchakato wa mazungumzo na ujifunzaji juu ya maana ya Ufunuo na utekelezaji wa maagizo yake kwa wanadamu katika Kipindi Kitakatifu, likiepukana na athari mbaya ya mabishano yasiyo na mwisho kuhusu maana na utendaji. Matokeo yake, uhusiano wenye uwiano kati ya watu binafsi, jumuiya na asasi hulindwa na kukuzwa katika njia yao sahihi, ambapo wote wanawezeshwa kufikia uwezo wao kamili na kutumia wakala na haki zao. Hivyo, jumuiya ya Kibahá'í huweza kusonga mbele kwa umoja na kuzidi kutimiza kusudi lake muhimu zaidi kupitia kuchunguza uhalisia na kuzalisha maarifa, kupanua ufikaji wa jitihada zake, na kuchangia kwenye maendeleo ya ustaarabu. Baada ya zaidi ya karne moja, ukweli wa uthibitisho wa `Abdu'l-Bahá unaonekana dhahiri zaidi: "mhimili wa umoja wa ulimwengu wa mwanadamu ni nguvu ya Agano na si kitu kingine".

Ukunjunjukaji wa Utaratibu wa Kiutawala

Zaidi ya uendelezaji wake wa Agano, Wasia na Agano la Abdul-Baha liliweka msingi kwa ajili ya mengine kati ya mafanikio muhimu sana ya karne ya kwanza ya Zama za Ujenzi: uibukaji na ukuaji wa Utaratibu wa Kiutawala, mtoto wa Agano. Katika karne moja, utawala, ambao ulianza na lengo la uanzishaji wa asasi za kuchaguliwa, ulikua katika mapana na utata, ukijitokeza ulimwenguni kote hadi ulipowaunganisha watu, nchi, na kanda zote. Maandiko ya Baha'u'llah na `Abdu`l-Bahá yaliyozianzisha asasi hizi pia yanatoa muono na mamlaka ya kiroho kwa asasi hizi kumsaidia mwanadamu katika kuujenga ulimwengu wenye haki na amani.

Kupitia Utaratibu wa Kiutawala wa Imani Yake, Bahá 'u'lláh amewahusisha watu binafsi, jamii, na asisi kama wahusika wakuu katika mfumo usio na mfano. Kufuatana na mahitaji ya zama za ukomavu wa binadamu, Yeye alifutilia mbali mazoea ya kihistoria ambapo makasisi walishikilia hatamu za mamlaka ya kidini wakiielekeza jumuiya ya waaminifu na kuongoza mambo yake. Ili kuzuia ushindani wa itikadi zinazoshindana; Yeye aliweka njia kwa ajili ya ushirikiano katika kutafuta ukweli na usitawi wa bindamu. Badala ya kutafuta madaraka juu ya wengine, Yeye alianzisha mipangilio ambayo ingekuza nguvu zilizofichika za watu binafsi na kujidhihirisha kwao katika huduma yenye manufaa kwa wote. Uaminifu, ukweli, uadilifu wa mwenendo, ustahimilivu, upendo na umoja ni miongoni mwa sifa za kiroho zinazounda msingi wa ushirika kati ya wahusika wakuu watatu wa njia mpya ya maisha, wakati juhudi kwa ajili ya maendeleo ya kijamii zote zinabumbwa na muono wa Bahá'u'lláh wa umoja wa binadamu.

Wakati wa kufariki kwa Abdul- Baha, asasi za imani zilikuwa na idadi ndogo ya mabaraza ya mahali yakifanya kazi kwa njia tofauti tofauti. Ni mawakala wachache tu waliofanya kazi mbali na ngazi ya mahali, na hakukuwa na mabaraza yoyote ya kiroho ya kitaifa. Bahá'u'lláh alikuwa amewateua Mikono wanne wa Hoja ya Mungu huko Iran, na Abdul-Bahá alielekeza shughuli zao kwa ajili ya maendeleo na ulinzi wa Imani, lakini hakuongeza idadi yao zaidi ya wanne waliokuwa

wameteuliwa baada ya kifo Chake. Hivyo, hadi wakati huo, Hoja ya Bahá'u'lláh, iliyojaa kiroho na uwezo usio dhahiri, bado haikuwa imeunda vyombo vya kiutawala ambavyo vingeiwezesha kupangilia juhudi zake.

Katika miezi ya mwanzoni ya utumishi wake, Shoghi Effend aifikiria kuanzisha Nyumba ya Haki ya Ulimwengu mara moja. Walakini, baada ya kutathmini hali ya Imani ulimwenguni kote, kwa haraka alihitimisha kwamba masharti yaliyokuwa yanahitajika kwa ajili ya uundwaji wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu yalikuwa bado hayajawekwa. Badala yake, aliwatia moyo Wabahá'i kila mahali kuweka nguvu zao katika kuinua mabaraza ya kiroho ya mahali na ya kitaifa. "Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa, kama vile nguzo, yataanzishwa hatua kwa hatua na kwa uthabiti katika kila nchi juu ya misingi yenye nguvu na iliyoimarishwa ya Mabaraza ya Mahali", yeye alisema. "Juu ya nguzo hizi, muundo wenye nguvu, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, itajengwa, ikiinua juu umbo lake tukufu juu ya ulimwengu wa uwepo."

Katika kuwasaidia marafiki kuelewa kazi yao katika ya kuweka misingi ya jumuiya yao, Shoghi Effend alilisisititiza kwamba Utaratibu wa Kiutawala haukuwa mwisho wake wenyewe, bali chombo cha kuelekeza roho ya Imani. Yeye alitilia mkazo mfumo wa tabia zake, akielezea kwamba utawala wa Kibahá'í "ni muundo wa kwanza tu wa kile kitakachokuja kuwa maisha ya kijamii katika siku zijazo na sheria za maisha ya jumuiya", na kwamba "waumini ndio tu wanaanza kuufahamu na kuutekeleza ipasavyo". Pia alieleza kwamba Utararibu wa Kiutawala ulikuwa ni "kiini na ruwaza" ya kile ambacho hatimaye kingekuja kuwa utaratibu mpya wa kupangilia masuala ya mwanadamu ulioonwa na Bahá'u'lláh. Na hivyo, kadiri marafiki walivyoanza kuuinua utawala, wangeweza kutambua kwamba uhusiano miongoni mwa watu binafsi, jumuiya na asasi zilizokuwa zinaanzishwa zingeendelea kubadilika katika utata, ukisababisha ukuaji wa uwezo wakati hadi wakati kadiri Imani ilivyopanuka na kuzalisha mtindo mpya wa maisha ambao daima ungeshirikisha, kwa upana zaidi watu wa ulimwengu.

Kupitia mabadilishano thabiti ya mawasiliano, Shoghi Effendi aliwaongoza marafiki hatua kwa hatua katika jitihada zao kujifunza kutumia mafundisho yanayohusiana na utawala, na kuongeza uelewa wao juu ya kusudi lake, ulazima wake, mbinu zake, umbo lake, kanuni zake, unyumbulifu wake, na namna ya uendeshaji wake, huku akiwathibitishia msingi dhahiri kwa masuala kama haya katika Maandiko ya Kibahá'í. Aliwasaidia katika kuendeleza mchakato wa chaguzi za Kibahá'í, uanzishwaji na usimamizi wa Mfuko wa Kibahá'í, maandalizi ya Mkutano Mkuu wa Kitaifa, ujengaji uhusiano kati ya Mabaraza ya Kitaifa na ya Mahali, na mambo mengine mengi. Aliondoa shaka na kusitasita kwa wale waliopambana kufahamu mwendelezo wa lazima kati ya utamaduni na mazoea ya maisha ya Kibahá'í wakati wa `Abdu'l-Bahá na hatua ambazo yeye, kama Mlinzi, alikuwa akichukua kuweka misingi ya kiutawala kwa ajili ya hatua inayofuata ya maendeleo ya Imani. Kadiri waumini walivyosimamia masuala yao ya kiutawala, kwa subira aliyajibu maswali yao, akisuluhisha matatizo, na kukuza maisha ya pamoja ya jumuiya ya ulimwengu wa Kibahá'í. Polepole, marafiki walijifunza kufanya kazi kwa upatano, kuunga mkono maamuzi ya asasi zao na kusaidia maendeleo yao, na kutambua kwamba vyote viwili, uelewa na uwezo wa kiutendaji ungeongezeka wakati hadi wakati. Mabaraza ya Mahali yalianza kufanya kazi kulingana na taratibu thabiti kwa ajili chaguzi, ushauriano, masuala ya kifedha, na mwenendo wa maisha ya jumuiya. Mwanzoni Mabaraza ya Kitaifa yalianzishwa katika visiwa vya Uingereza, Ujerumani

na Austria, India na Burma, Misri na Sudan, Caucasus, Turkistan, na Marekani na Canada. Kufuatana na asili ya mfumo wa Utaratibu wa Kiutawala, Mabaraza ya Kitaifa aghalabu yalianzishwa kwanza kwenye ngazi ya kanda, yakijumuisha zaidi ya nchi moja, na baadaye tu kwenye ngazi ya kitaifa au majimbo kadiri idadi ya waumini na Mabaraza ya Mahali ilivyoongezeka. Katika mkondo wake, kamati nyingi mbalimbali ziliundwa, zikiteuliwa kwenye ngazi zote mbili; ya mahali na ya kitaifa, kuendeleza jitihada zao za pamoja katika maeneo mbalimbali yakiwemo ufundishaji, tafsiri, uchapishaji, elimu, utangulizi, na uandaaji wa Karamu za Siku Kumi na Tisa na Siku Takatifu.

Baada ya miongo mitatu ya kujidhatiti kujenga utawala kwenye ngazi ya mahali na kitaifa, katika miaka ya mwisho ya uhai wake Shoghi Effendi alizindua hatua mpya katika uendelezaji wa Utaratibu wa Kiutawala kwa kuleta kuanzisha asasi kwenye ngazi za kimataifa na kibara. Ilianza na "matarajio yaliyosubiriwa kwa muda mrefu ya uinuaji na uanzishaji wa Makao Makuu ya Kiutawala ya Ulimwengu ya Imani ya Bahá'u'lláh katika Nchi Takatifu". Mwaka 1951, yeye alitangaza uundwaji wa Halmashauri ya Kibahá'í ya Kimataifa. Asasi hii mpya, alielezea, ingebadilika kupitia hatua mbalimbali kwa ajili ya maandalizi ya ubadilikaji na uchanuaji wake kuwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.

Maendeleo haya makubwa punde yalifuatwa, mwishoni mwa mwaka huo huo, na uteuzi wa Shoghi Effendi wa Mikono kumi na wawili wa Hoja wa Mungu, ikiwakilishwa sawa sawa katika mabara matatu na Nchi Takatifu—kikosi cha kwanza cha Mikono wa Hoja kiliinuliwa kwa kufuatana na maagizo ya Wasia na Agano la `Abdu'l-Bahá. Watu hawa wa heshima waliteuliwa kuendeleza kazi ya uenezaji na ulinzi wa Imani. Uwepo wa asasi inayotekeleza jukumu muhimu kama hilo katika uendelezaji wa raghba za Hoja, lakini ambayo haina mamlaka ya utungaji sheria, ya utendaji, au ya kimahakama na isiyo na kazi za ukasisi au haki ya kutoa fasiri zenye mamlaka, ni sura ya utawala wa Kibahá'í isiyolinganishwa katika dini za zamani. Baada ya miaka mingi ya kulea mfumo wa Mabaraza yaliyochaguliwa na mawakala wao husika, Shoghi Effendi alianza kuunda asasi hii iliyoteuliwa, na kuwaongoza marafiki kuelewa, kupokea, na kusaidia kazi zake za kipekee. Uteuzi wa kikosi cha pili cha Mikono mnamo 1952, ulipandisha idadi yao kufikia kumi na tisa. Bodi za Wasaidizi, ambazo wajumbe wao walihudumu kama manaibu wa Mikono katika kila bara, zilianzishwa mwaka 1954. Hata hadi siku za mwisho wa uhai wake, Mlinzi aliendelea kuipanua asasi hii, akiteua kikosi cha mwisho cha Mikono kuongeza idadi yao hadi ishirini na saba, na kuanzisha Bodi ya Wasaidizi kwa ajili ya ulinzi ili kushamirisha Bodi ya Uenezaji.

Katika kutafakari juu ya juhudi zao za kujenga umbo changa la utawala, Shoghi Effendi alikuwa amewaelezea waumini kwamba mengi ya yale yaliyoanzishwa chini ya mwongozo wake yalikuwa ya muda na kwamba ilikuwa ni kazi ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu "kuweka dhahiri zaidi kile ambacho lazima kiongoze shughuli za siku zijazo na utawala" za Imani. Mahali pengine aliandika kwamba "Chombo hiki Kikuu Kabisa kitakapokuwa kimesimikwa barabara, kitatakiwa kuzingatia upya hali yote, na kuweka kanuni itakayoelekeza, ilimradi itaona inafaa, masuala ya Hoja".

Kufuatia kifo kisichotarajiwa cha Shoghi Effendi Novemba 1957, jukumu la mambo ya Hoja kwa kipindi kifupi liliangukia kwenye Mikono wa Hoja ya Mungu. Mwezi mmoja tu kabla walikuwa wameteuliwa na Mlinzi kama "Wasimamizi Wakuu wa Jumuiya changa ya madola ya Ulimwengu wa Baha'u'llah, ambao wamejaliwa na kalamu isiyokosea ya Kitovu cha Agano Lake kazi maradufu ya kulinda usalama, na ya kuhakikisha uenezaji, wa Imani ya Baba Yake". Mikono hawa walifuata kwa uaminifu na bila kubadili msimamo njia iliyowekwa na Mlinzi. Chini ya usimamizi wao, idadi ya Mabaraza ya Kitaifa iliongezeka kutoka ishirini na sita hadi hamsini na sita, na hadi kufikia 1961 hatua ambazo alikuwa amezieleza kwa ajili ya mpito wa Halmashauri ya Kibahá'í ya Kimataifa kutoka kuwa chombo kilichoteuliwa mpaka kile kilichochaguliwa zilikuwa zimetekelezwa, wakiandaa njia kwa ajili ya uchaguzi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu mwaka 1963.

Ukunjukaji hai wa utawala, uliokuzwa kwa uangalifu sana na Mlinzi, uliendelezwa kwa mpangilio na kupanuliwa zaidi chini ya maelekezo ya Nyumba ya Haki. Muda uliofuata wa zaidi ya nusu karne ulishuhudia mafanikio makubwa. Miongoni mwa yale yaliyojipambanua kati ya haya, Katiba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, iliyosifiwa na Mlinzi kama "Sheria Kuu Kabisa", ilipitishwa mnamo 1972. Baada ya ushauriano na Mikono wa Hoja, kazi za asasi hiyo zilipanuliwa katika wakati ujao kupitia uundaji wa Bodi za Washauri za Bara mwaka 1968 na wa Kituo cha Ufundishaji cha Kimataifa mwaka 1973. Aidha, kwa mara ya kwanza, Washauri Wasaidizi waliidhinishwa kuteua wasaidizi ili kupanua ufikiaji wa utumishi wao kwa ajili ya uenezi na ulinzi kwenye ngazi ya chini. Idadi ya Mabaraza ya Kitaifa na ya Mahali iliongezeka na uwezo wao kutumikia jumuiya ya Kibahá'í na kupanua ushawishi wao kupitia kujihusisha na jamii pana zaidi ulikuzwa. Halmashauri za Kibahá'í za Kanda zilianzishwa mwaka 1997 kusaidia kushughulikia utata ulioongezeka wa masuala yaliyoyakabili Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa huku zikidumisha urari kati ya utawala wa kati na ugatuaji katika masuala ya kiutawala ya jumuiya.

Mfumo wa kamati za ufundishaji ulioanzishwa wakati wa Mlinzi pole pole ulitoa nafasi kwa ajili ya miundo ambayo ingeweza kuchukua majukumu ya upangaji na ufanyaji maamuzi kwenye ngazi zilizogatuliwa zaidi, ukipenya mbali zaidi hadi kwenye ujirani na vijiji. Zaidi ya asasi mia tatu za mafunzo, zaidi ya Halmashauri mia mbili za Kanda, na mipangilio ya kiutawala katika zaidi ya klasta elfu tano ilianzishwa. Kwenye Ridván 1992 sheria ya Huqúqu'lláh ilitumika kwa wote katika ulimwengu wa Kibahá'í na muundo wake wa kiasasi baadaye kuimarishwa kupitia uanzishwaji wa mtandao wa Bodi za Wadhamini na Wawakilishi kwenye ngazi ya kanda na ya kitaifa, hali kadhalika, mwaka 2005, kupitia uteuzi wa Bodi ya Kimataifa ya Wadhamini. Kufuatia kifo cha Shoghi Effendi, ujenzi wa Mashriqu'l-Adhkár huko Uganda, Australia, Ujerumani, na Panama ulikamilishwa, na zingine hatimaye ziliinuliwa huko Samoa, India na Chile; mnamo 2012, mchakato wa uanzishwaji wa Nyumba za Ibada ulipanuliwa kwenye ngazi za kitaifa na za mahali.

Zaidi ya karne, basi, kupitia mfululizo wa hatua za kimaendeleo, uhusiano miongoni mwa watu binafsi, jumuiya na asasi umeendelea kubadilika na kukua hadi kuwa maumbo tata zaidi, na misingi ya utawala imepanuliwa, mbinu zake kuendelea kurekebishwa, na mipangilio ya ushirikiano kubainishwa na kuendelea kuboreshwa. Kile kilichoanza mwanzoni mwa karne ya kwanza ya Zama za Ujenzi kama mtandao wa vyombo vilivyochaguliwa kikawa, hadi mwishoni mwa karne hiyo, kundi kubwa mno la asasi na wakala linaloanzia ngazi ya chini hadi ngazi ya

kimataifa, likiuunganisha ulimwengu wa Kibahá'í katika mawazo na vitendo ndani ya shughuli ya pamoja katika mikutadha ya tamaduni anuai na mipangilio ya kijamii.

Leo, ingawa utawala bado haujafikia ukomavu wake kamili, mfumo uliozinduliwa na Bahá'u'lláh hudhihirisha mtindo mpya wa mwingiliano na nguvu ya kushangaza katika uhusiano miongoni mwa wahusika wakuu watatu wanapojishughulisha na kusudi la pamoja la kufanya kazi kwa ajili ya mfumo wa maendeleo ya Imani na uboreshaji wa ulimwengu. Wakiwa na watenda-kazi wenza wenye mwelekeo sawa na katika hali mbalimbali za ujifunzaji, tafakari, na mwingiliano mwingi wa kijamii, watu binafsi hutoa mawazo yao na hutafuta ukweli kupitia mchakato wa ushauriano, bila kusisitiza juu ya usahihi wa mawazo yao wenyewe. Kwa pamoja, wanasoma uhalisia wa mazingira yao, kuchunguza vilindi vya mwongozo uliopo, kuchota umaizi husika kutoka Mafundisho na kutoka tajiriba iongezekayo, kuunda mazingira shirikishi na yainuayo kiroho, kujenga uwezo, na kuanzisha vitendo ambavyo hukua katika ufanisi na utata kadiri muda upitavyo. Wanajaribu kutofautisha yale maeneo ya shughuli ambamo mtu binafsi huweza kutekeleza vyema kabisa uanzishaji wa jambo kutokana na yale yanayoangukia kwenye asasi pekee, na kwa nguvu zote wanakaribisha mwongozo na mwelekeo wa asasi zao. Katika klasta zilizopiga hatua na ndani ya vijiji na ujirani ambavyo ni vituo vya shughuli shadidi, jumuiya huibuka na hisia ya utambulisho wa pamoja, nia na madhumuni, ikitoa mazingira ya kulea uwezo wa watu binafsi na kuwaunganisha katika mlolongo wa shughuli zinazokamilishana na zinazoimarisha pande zote ambazo huwakaribisha wote na kutafuta kumtia moyo kila mtu. Jumuiya kama hizi zinazidi kupambanuliwa kwa hisia ya umoja miongoni mwa wana-jumuiya wao, uhuru wao kutokana na chuki za aina zote, tabia yao ya kiibada, kujitoa kwao kwa usawa wa wanawake na wanaume, huduma yao isiyo na ubinafsi kwa wanadamu, michakato yao ya kielimu na ukuzaji wa njema, na uwezo wao wa kujifunza kwa mpangilio na kuchangia kwenye maendeleo ya kimwili, ya kijamii na ya kiroho ya jamii. Wale wana-jumuiya wanaoitwa kutoa huduma kwenye asasi wanajitahidi kujifahamisha juu ya wajibu wao kuweka kando wanayoyapendelea na wasiyoyapendelea wenyewe, kamwe kujiona wenyewe kuwa mapambo makuu ya Hoja au kuwa bora kuliko wengine, na kujiepusha na jaribio lolote la kudhibiti mawazo na matendo ya waumini. Katika kutekeleza majukumu yao, asasi huwezesha mabadilishano ya kiubunifu na kiushirikiano miongoni mwa vipengele vyote vya jumuiya na kujitahidi kupata muafaka, kuzishinda changamoto, kukuza siha ya kiroho na uchangamfu, na kuamua kupitia tajiriba njia zenye ufanisi zaidi za kufuatilia malengo na makusudi ya jumuiya. Kupitia njia mbalimbali, ikiwemo uanzishwaji wa mawakala wa kielimu, wanasaidia kukuza maendeleo ya kiroho na ya kiakili ya waumini.

Kama matokeo ya uhusiano huu mpya na uwezo wa wahusika wakuu watatu, duara la wale wenye uwezo wa kufikiri na kutenda kimkakati limepanuka, ambapo msaada, rasilimali, hamasa, na mwongozo wa upendo hupanuliwa popote vinapohitajika. Tajiriba na umaizi vinasambazwa kote ulimwenguni, kutoka chini kabisa hadi ngazi ya kimatifa. Mtindo wa maisha ulioundwa na uhusikaji huu wenye nguvu hukumbatia mamilioni ya roho kutoka nyanja zote za maisha, zikihuishwa na muono wa Bahá'u'lláh wa ulimwengu uliounganika. Katika nchi hadi nchi, umevuta umakini wa wazazi, walimu, viongozi wa kimila, maofisa, na viongozi wenye fikra kwenye mamlaka ya mfumo wake kushughulikia mahitaji ya haraka ya ulimwengu. Kwa kawaida, si kila jumuiya huonesha sifa za ile iliyopiga hatua zaidi; kwa hakika, katika historia ya Kibahá'í

hii daima imekuwa hivyo. Walakini, utokeaji wa uwezo mpya katika sehemu yoyote ile huashiria maendeleo ya wazi na hutumika kama ubashiri kwamba mwingine kwa hakika utafuata njia hiyo.

Katika vipindi na karne zijazo, Utaratibu wa Kiutawala utaendeleza mabadiliko ya mfumo wake katika kuitikia kwenye ukuaji wa Imani na kwenye mahitaji ya jamii ibadilikayo. Shoghi Effendi alitazamia kwamba kadiri "vipengele vya sehemu zake, mfumo wake wa asasi, uanzavyo kufanya kazi kwa ufanisi na bidii," Utaratibu wa Kiutawala "utathibitisha dai lake na kuonesha uwezo wake kufikiriwa si tu kama kiini ila ndiyo mtindo wenyewe wa Utaratibu mpya wa Ulimwengu unaokusudia kuwakumbatia wanadamu wote katika utimilifu wa wakati. Hivyo, kadiri mfumo wa Bahá'u'lláh uundwavyo, utaipa jamii ya binadamu njia mpya na zenye manufaa zaidi za kupangilia masuala yake. Wakati wa mabadailiko haya ya kimfumo, uhusiano miongoni mwa watu binafsi, jumuiya, na asasi utakunjuka bila kuepukika katika mielekeo mipya na wakati mwingine kwa njia zisizotarajiwa. Hata hivyo, ulinzi mtakatifu usioshindwa ambao huizunguka Nyumba ya Haki utahakikisha kwamba, kadiri ulimwengu wa Kibahá'í unavyotafuta njia yake kapitia msukosuko wa kipindi chenye hatari zaidi katika mabadiliko endelevu ya kijamii ya wanadamu, utafuata, bila kukengeuka, mwelekeo uliowekwa na Mjalia.

Ueneaji na maendeleo ya Imani Ulimwenguni

Tangu mwanzo wake, jumuiya iliyoinuliwa na Bahá'u'lláh, ingawa ni ndogo kiidadi na yenye mipaka kijiografia, ilitiwa nguvu na mafundisho Yake bora na iliinuka kushiriki kwa uhuru na wale wote waliotafuta njia ya kiroho kuelekea mabadiliko binafsi na ya kijamii. Kadiri muda ulivyopita, marafiki walijifunza kufanya kazi kwa karibu na watu wenye mwelekeo unaofanana nao na mashirika ya kuinua roho ya binadamu na kuchangia kwenye uboreshaji wa familia, jumuiya, na jamii kwa jumla. Upokevu kwa ujumbe wa Bahá'u'lláh ulipatikana kila mahali, na kupitia juhudi za kujidhatiti na za kujitoa dhabihu kwa vizazi vingi, jumuiya za Kibahá'i ziliibuka ulimwengu mzima, kwenye miji na vijiji vya mbali, ikijumuisha anuai ya mbari ya binadamu.

Katika Kipindi Kitakatifu cha Báb, Imani ilianzishwa katika nchi mbili. Wakati wa Bahá'u'lláh ilipanuka hadi jumla ya nchi kumi na tano, na kufikia mwisho wa utumishi wa 'Abdu'l-Bahá ilikuwa imefikia kwenye nchi thelathini na tano hivi. Wakati wa kipindi cha machafuko ya vita vya dunia, 'Abdu'l-Bahá alifunua mojawapo ya urithi wake wenye thamani isiyokadirika, Nyaraka za Mpango Mtakatifu, mpango Wake mkuu kwa ajili ya uangaziaji wa kiroho wa sayari kupitia uenezaji wa mafundisho ya Bahá'u'lláh. Hati hii yenye thamani iliinua mwito kwa ajili ya jitihada za pamoja na za kimkakati; hata hivyo, hadi kufikia kipindi cha kupaa kwa Bwana, ulikuwa umepenyeza kwa shida mawazo na vitendo vya jumiya, na ni mashujaa wachache tu wasio wa kawaida wa Imani, Martha Root akiwa mstari wa mbele miongoni mwao, waliinuka kuuitikia.

Kwa miaka ishirini baada ya kufunuliwa kwa Nyaraka za Mpango Mtakatifu kwa kalamu ya 'Abdu'l-Bahá, utekelezwaji wake ulisimamishwa kwa muda hadi kipindi ambapo marafiki, wakiongozwa na Shoghi Effendi, wangeweza kuunda vyombo vya kiutawala vya Imani na kukuza utendaji-kazi wake ufaao. Ni pale tu muundo wa awali wa kiutawala ulipowekwa thabiti ndipo Mlinzi angeweza kuanza kufafanua muono wa ufungukaji wa Imani kulingana na Mpango Mtakatifu wa 'Abdu'l-Bahá. Kama ambavyo utawala ulivyobadilika kupitia hatua bainifu za uongezekaji utata, vivyo hivyo ndivyo jitihada za kushiriki na kutumia mafundisho ya Bahá'u'lláh

pole pole ilivyobadilika, ikiibua mitindo mipya ya maisha ya jumuiya ambayo daima ingeweza kukumbatia idadi kubwa zaidi, kuwawezesha marafiki kukabiliana na changamoto kubwa zaidi, na kuchangia kwenye kiwango kilichoongezeka cha mabadiliko binafsi na ya kijamii.

Kuanza jitihada hii ya kimpangilio, Shoghi Effendi aliziagiza jumuiya za Marekani na Canada—wapokeaji wateule wa Nyaraka za Mpango Mtakatifu, ambao aliwataja, mtawalia, kama watekelezaji wakuu na washirika wao—kuunda "mpango wenye utaratibu, uliotungwa kwa umakini, na ulioanzishwa vyema" ambao ulitakiwa "kutekelezwa kwa bidii na kuendelea kupanuliwa". Mwito huu ulisababisha uzinduzi wa Mpango wa kwanza wa Miaka Saba mwaka 1937, ambao ulipeleka mafundisho ya Bahá'u'lláh huko Amerika Kusini, ukifuatiwa na Mpango wa pili wa Miaka Saba, ulioanza mwaka 1946, ambao ulisisitiza maendeleo ya Imani huko Ulaya. Shoghi Effendi pia alihimiza kazi ya ufundishaji kwenye jumuiya zingine za kitaifa, ambazo baadaye zilipitisha mipango ya kitaifa chini ya jicho lake angalifu. Baraza la Kiroho la Kitaifa la India na Burma lilipitisha mpango wake wa kwanza mwaka 1938; Visiwa vya Uingereza 1944; Uajemi 1946; Australia na New Zealand 1947; Iraq 1947; Canada, Misri na Sudan, na Ujerumani na Austria mwaka 1948; na Amerika ya Kati 1952. Kila moja ya mipango hii ulifuata ruwaza sawa sawa ya kimsingi: kufundisha watu binafsi, kuanzisha Baraza la la Mahali na kuinua jumuiya, na kufungua maeneo zaidi eneo la nyumbani au katika nchi zingine—na kisha kurudia ruwaza kwa mara nyingine tena. Wakati msingi thabiti ulipojengwa katika nchi au eneo, Baraza jipya la Kitaifa lingeweza kuanzishwa.

Wakati wa miaka hii, Shoghi Effendi daima aliwahamasisha marafiki kutekeleza jukumu lao la kufundisha Imani ndani ya muktadha wa mipango iliyopitishwa na Mabaraza yao ya Kitaifa. Baada ya muda, mbinu kama vile utangulizi, walimu wasafiri, mikusanyiko ya fayasaidi, shule za kiangazi, na ushiriki kwenye shughuli za mashirika yenye mwelekeo unaofanana zilithibitisha kuwa zenye ufanisi kwenye maeneo fulani, na aliwasihi marafiki sehemu zingine za ulimwengu kuzitumia. Jitihada za upanuzi zilioanishwa na msisitizo juu ya maendeleo ya ndani yahitajikayo ili kuimarisha utambulisho na hulka ya Imani ya Kibahá'í kama jumuiya bainifu ya kidini. Mchakato huu wa ubadilishaji ulilelewa kwa uangalifu na Mlinzi, ambaye aliwaeleza waumini historia ya Imani yao, alirahisisha matumizi ya kalenda ya Kibahá'í, alisisitiza ushiriki wa mara kwa mara kwenye Karamu na uadhimishaji wa Siku Takatifu, na kwa subira aliwaongoza kukumbatia wajibu wa utiifu kwa sheria za Kibahá'í, kama vile maagizo ya ndoa ya Kibahá'í. Pole pole, Imani iliibuka kama dini ya ulimwengu, ikichukua nafasi yake miongoni mwa dini zake pacha.

Sambamba na uzinduzi wa asasi za kimataifa, jitihada za pamoja za Imani kwenye uga wa ufundishaji zilienda hadi kwenye uwanja wa ushirikiano wa kimatatifa. Mwaka 1951, jumuiya tano za kitaifa zilishirikiana kwenye utekelezaji wa kampeni ya kiafrika "yenye matarajio ya juu" na "umuhimu wa kina" kuzidisha usambaaji wa Imani kwenye bara hilo zima. Na mwaka 1953, Mpango wa Mapambano ya Miaka Kumi ulianzishwa, ukiunganisha jitihada za Mabaraza yote kumi na mawili ya Kitaifa kwenye mpango mmoja wa pamoja wa ulimwengu—wa kwanza wa aina yake. Katika hatua hii ya kilele ya utumishi wa Mlinzi, mtandao wa vyombo vya kiutawala ambavyo marafiki waliviinua na mbinu za ufundishaji zilizothibitishwa walizozikuza zilitumiwa

kwenye shughuli ya pamoja ya kiroho ambayo mfano wake jumuiya ya Kibahá'í kamwe haikuwahi kushuhudia hapo kabla.

Kadiri waumini walivyosafiri mbali na kwa mapana kushiriki Imani yao yenye thamani, walikuta miongoni mwa jamii mbalimbali za watu upokevu wa kanuni na mafundisho yake. Watu hawa waligundua ndani ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh maana ya kina zaidi na kusudi la maisha yao, hali kadhalika umaizi mpya ambao ungewezesha jumuiya zao kuzishinda changamoto na kuendelea kiroho, kijamii, na kimwili. Mwanga mtakatifu, ulioenezwa taratibu hapo awali kutoka mtu hadi kwa mtu, hivyo ulianza kuenezwa kwa haraka miongoni mwa umma wa wanadamu. Ile dalili ya tukio la uingiaji kwa makundi iliyotabiriwa na Abdu'l-Bahá ikawa imeithibitishwa katika uandikishaji wa mamia ya waumini huko Uganda, Gambia, visiwa vya Gilbert na Ellice, na baadaye, Indonesia na Cameroon. Kabla Mpango huo haujaisha, mchakato huo ulikuwa umeanza kwenye nchi zingine kadhaa, na wale watu walioikumbatia Imani wakifikia hadi makumi ya maelefu au hata zaidi.

Baada ya kufariki kwa Shoghi Effendi, Mikono wa Hoja walihakikisha uhitimishwaji wenye mafanikio wa Mpango wa Mapambano ya Miaka Kumi kwa kufuata bila kukengeuka njia aliyoiainisha. Kwa kutumia masomo waliyojifunza chini ya uongozi wa Mlinzi, mengi zaidi yalitimizwa kwenye uga wa ufundishaji kwa kipindi cha muongo mmoja kuliko karne iliyopita. Imani ilienea kwenye nchi mpya na majimbo 131, na idadi ya mahali ambapo Wabahá'í waliishi ilivuka elfu kumi na moja, ikiwa na jumla ya Mabaraza ya Kiroho ya Kitaifa hamsini na sita na zaidi ya Mabaraza ya Mahali 3,500. Shughuli hii ilihitimishwa kwa kuchaguliwa kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na wajumbe wa Mabaraza hayo ya Kitaifa, kulingana na maagizo yaliyowekwa na 'Abdu'l-Bahá.

Baada ya kuanziswa kwake, Nyumba ya Haki ya Ulimwengu iliendeleza utekelezaji wenye mpangilio wa Mpango Mtakatifu, ikizindua kipindi chake cha pili kwa kupanua pole pole na kuongeza mlolongo wa shughuli zilizolelewa na Mlinzi, ikiongezea kwenye, au kuendeleza vipengele mbalimbali vya kazi, na kuratibu na kuunganisha shughuli za Mabaraza yote ya Kitaifa. Miongoni mwa maeneo ya msisitizo yaliyoibuka au kupata uangalifu ulioongezeka ilikuwa ni ushiriki wa pamoja wa watu binafsi katika huduma kwa Hoja na uimarishaji wa uelewa wa watu binafsi wa sheria na mafundisho. Aidha, mchakato wa kuimarisha asasi ulisisitiza ushirikiano baina ya Bodi za Washauri ambazo ndiyo tu zilikuwa zimeanzishwa na Mabaraza ya Kitaifa, hali kadhalika baina ya Washauri Wasaidizi na Mabaraza ya Kiroho ya Mahali. Maisha ya jumuiya yaliimarishwa kupitia mkazo kwenye madarasa ya watoto, uanzishwaji wa shughuli kwa ajili ya vijana na wanawake, na kufanya mikutano ya Baraza ya mara kwa mara. Mikakati mingine ilihusisha utangazaji mpana wa Imani na uendelezaji wake kupitia vyombo vya habari; ukuzaji wa vituo vya ujifunzaji, zikiwemo shule za kiangazi na taasisi za ufundishaji; ujihusishaji mkubwa kwenye maisha ya jamii; na ulelewaji wa uanazuoni wa Kibahá'í.

Kama matokeo ya jitihada zote hizi, hadi kufikia miaka ya 1990 Imani ilikuwa imeenea kwenye makumi ya maelfu ya maeneo na idadi ya Mabaraza ya Kitaifa iliongezeka zaidi ya mara tatu hadi kufikia takribani 180. Katika kipindi hiki, ukuaji wa jumuiya za kitaifa ulifuata ruwaza mbili pana ambazo kwa sehemu kubwa ulitegemea juu ya mwitikio wa jamii pana. Katika ile ya kwanza, jumuiya za mahali zilielekea kuwa ndogo kwa ukubwa, na baadhi tu zilikua hadi kufikia idadi ya

waumini mamia au zaidi. Jumuiya hizi mara nyingi zilipambanuliwa kwa mchakato imara wa uimarishaji ambao uliwezesha upeo mpana wa shughuli na uibukaji wa hisia ya nguvu ya utambulisho wa Kibahá'í. Hata hivyo, iliendelea kuwa dhahiri zaidi kwamba, ingawa ziliungana katika imani ya pamoja, zilizopambanuliwa kwa maadili bora kabisa, na yenye uwezo wa kumudu masuala yake na kufikia kwenye mahitaji yake, jumuiya ndogo kama hiyo—hata ingesitawi namna gani au kujaribu kuwahudumia wengine kupitia jitihada zake za kibinadamu—kamwe isingetumaini kuwa kama mfano wa uundaji upya wa jamii nzima.

Ruwaza ya pili ilipata umbo kwenye zile nchi ambako mchakato wa uingiaji kwa makundi ulianza, ukisababisha ongezeko la haraka mno la idadi ya waumini, maeneo mapya, na asasi mpya. Katika nchi kadhaa jumuiya ya Kibahá'í ilikua ikijumuisha zaidi ya waumini laki moja, ambapo India ilifikia kama milioni mbili hivi. Kwa hakika, katika kipindi kimoja cha miaka miwili ya mwishoni mwa 1980, zaidi ya roho milioni moja ziliikumbatia Imani ulimwenguni kote. Bado, katika maeneo hayo, licha ya jitihada za kiubunifu na za kujitoa dhabihu zilizofanywa, mchakato wa uimarishaji haukuweza kuendana na upanuzi. Wengi wakawa Wabahá'í lakini njia hazikuwepo kwa waumini wapya wote hawa kuimarishwa vya kutosha kwenye kanuni za msingi za Imani na kwa ajili ya jumuiya hai kukua. Madarasa ya elimu ya Kibahá'í hayakuweza kuanzishwa kwa idadi kubwa kutosha kuhudumia idadi iongezekayo daima ya watoto na vijana. Zaidi ya Mabaraza ya Mahali elfu thelathini yaliundwa, lakini ni sehemu tu ya hayo yalianza kufanya kazi. Kutokana na tajiriba hii, ilikuwa dhahiri kwamba kozi za mara moja moja za kielimu na shughuli zisizo rasmi za jumuiya, ingawa ni muhimu, hazikutosheleza, kwa kuwa zilisababisha kuinua kundi dogo tu la wasaidizi hai wachache wa Hoja ambao, haidhuru ni kwa kiasi gani walivyojitoa, wasingeweza kukidhi mahitaji ya maelfu kwa maelefu ya waumini wapya.

Hadi kufikia 1996 ulimwengu wa Kibahá'í ulikuwa umefikia hatua ambapo maeneo mengi ya shughuli ambayo hapo awali zilichangia kwenye maendeleo makubwa kama hayo kwa kipindi cha miaka mingi yalihitaji kutathiminiwa na kuelekezwa upya. Watu binafsi, jumuiya, na asasi hawakuhitaji tu kujifunza namna ya kuanzisha mtindo wa utendaji ambao ungeifikia idadi kubwa, bali pia jinsi ya kuongeza kwa haraka idadi ya watu binafsi ambao wangeweza kushiriki kwenye vitendo vya huduma ili kwamba uimarishaji uendane na upanuzi uchapuzwao. Jitihada ya kuitambulisha Imani kwenye jamii nyingi za watu wa ulimwengu ililazimika iwe yenye mpangilio zaidi. Mwito wa Mpango wa Miaka Minne kwa "maendeleo makubwa katika mchakato wa uingiaji kwa makundi" ulikusudiwa kukiri kwamba mazingira ya Imani, pamoja na hali za jamii ya wanadamu, ziliruhusu, na hata kuhitaji, ukuaji endelevu wa jumuiya ya ulimwengu wa Kibahá'í kwa kiwango kikubwa. Ni hapo tu ndipo nguvu ya mafundisho ya Bahá`u`lláh ya kubadili hulka ya binadamu ingeweza kutambulika zaidi.

Mwanzoni mwa Mpango wa Miaka Minne, marafiki katika kila kanda walihamasishwa kubaini mbinu na njia ambazo zilifaa kwa hali zao mahsusi na kuanzisha mchakato wenye mpangilio wa maendeleo ya jumuiya ambao kwayo wangepitia tena mafanikio yao na changamoto, kurekebisha na kuboresha mbinu zao ipasavyo, kujifunza, na kusonga mbele bila kusita. Wakati njia ya kiutendaji haikuwa wazi, mlolongo wa mbinu kwenye changamoto mahsusi zilizobainishwa na Mpango zingeweza kujaribiwa katika maeneo tofauti tofauti; wakati jitihada kwenye eneo fulani ilipothibitisha, kupitia tajiriba, kuwa yenye kufaa, vipengele vyake vingeweza kushirikishwa na

asasi kwenye ngazi ya kitaifa au kimataifa na kisha kusambazwa kwenye maeneo mengine na hata kuwa sehemu ya Mipango ijayo.

Kwa zaidi ya robo karne mchakato huu wa ujifunzaji kuhusu ukuaji ulisababisha kuibuka kwa mlolongo wa dhana, vyombo, na mbinu ambazo ziliendelea kuimarisha muundo ubadilikao wa kiutendaji wa jumuiya. Miongoni mwa vipengele hivi mashuhuri ilikuwa ni uundaji wa mtandao wa taasisi za mafunzo—zikitoa programu za elimu kwa watoto, vijana chipukizi, na vijana na watu wazima—kwa kuwawezesha marafiki kwa idadi kubwa na kuwasaidia kuongeza uwezo wao wa kuhudumu. Vingine ilikuwa ni dhana ya klasta, ambayo ilirahisisha upangiliaji wa kazi ya ufundishaji kwenye maeneo ya kijiografia yanayoweza kusimamiwa kupitia uanzishaji na uimarishaji wa pole pole wa programu za ukuaji, na kuongeza kasi ya uenezaji na ukuaji wa Imani ndani ya kila nchi na ulimwengu mzima. Ndani ya programu za ukuaji kama hizi, mtindo mpya wa maisha ya jumuiya uliibuka, ukianzia na uongezekaji wa shughuli za msingi nne ambazo zilitumika kama milango kwa ajili ya uingiaji wa idadi kubwa, ukiunganishwa na mlolongo wa jitihada zingine, ikiwemo ufundishaji wa watu binafsi na wa pamoja, ziara za majumbani, kukarimu mikusanyiko ya kijamii, kuadhimisha Karamu na Siku Takatifu, kusimamia masuala ya jumuiya, na kukuza shughuli kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi—ambapo zote hizi kwa pamoja zingeleta mabadiliko kwenye tabia ya kiroho ya jumuiya na kuimarisha vifungo vya kijamii miongoni mwa watu binafsi na familia.

Tukitazama nyuma kwenye karne ya jitihada ya kutekeleza maagizo ya Mpango Mtakatifu, inakuwa wazi kwamba ulimwengu wa Kibahá'í umepitia maendeleo makubwa kwenye ngazi ya utamaduni. Idadi kubwa daima zimejihusisha katika mchakato wa ujifunzaji kwa utashi kutumia Mafundisho yahusuyo ukuaji na maendeleo ndani ya muundo wa utendaji ambao unabadilika kupitia tajiriba ya marafiki na mwongozo wa Nyumba ya Haki. Ongezeko katika uwezo kwa ajili ya kujihusisha katika mchakato huu wa ujifunzaji ni dhahiri katika sifa ambazo zinaendelea kudhihirika katika jumuiya ya Kibahá'í: kudumisha mwelekeo wa unyenyekevu wa ujifunzaji, wawe wanasherehekea mafanikio au wakivumilia mbele ya vikwazo na vizuizi; wakiimarisha utambulisho wa Kibahá'í wakati huo huo wakilinda mazingira rafiki kwa wote; na daima wakitenda katika nyanja pana zaidi za jitihada wakati huo huo wakiendelea kuimarisha mbinu kwa kazi ya Hoja ambayo ni yenye mpangilio na mfungamano. Kwenye maelfu ya klasta, idadi iongezekayo ya watu wamejiona kama wahusika wakuu katika upatanaji, uzalishaji, na utumiaji wa maarifa kwa ajili ya ukuaji na maendeleo yao. Wanajihusisha katika majadiliano kama familia, marafiki, na jamaa juu ya dhana zilizoadilishwa za kiroho na masuala yenye umuhimu wa kijamii; wakianzisha shughuli ambazo hubumba mtindo wa Maisha uliopambanuliwa kwa sifa yake ya kiibada; wakitoa elimu kwa vijana wadogo na kuongeza uwezo wao wa kuhudumu; na kuchangia kwenye maendeleo ya kimwili na ya kijamii ya jumuiya zao. Wanawezeshwa kuchangia kwenye uboreshaji wa jumuiya yao ya mahali na ulimwengu kwa jumla. Kadiri wanavyofikiria na kutenda kwa namna hii, wamepata utambuzi wa kina zaidi wa kusudi la dini yenyewe.

Kujihusisha na maisha ya jamii

Bado kipengele kingine cha ukunjukaji wa Mpango Mtakatifu wa `Abdu'l-Bahá ni uhusikaji mkubwa zaidi wa jumuiya ya Kibahá'í katika maisha ya jamii. Tangu mwanzo wa utumishi wake, Shoghi Effendi aliteka umakini wa marafiki tena na tena juu ya nguvu ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh

kuathiri mabadiliko ya kimfumo katika jamii—mchakato ambao hatimaye ungesababisha uibukaji wa ustaarabu wa kiroho. Wabahá'i, kwa hiyo, iliwabidi kujifunza kuyatumia mafundisho ya Bahá'u'lláh si tu kwa ajili ya mabadiliko binafsi ya kiroho bali pia kwa ajili mabadiliko ya kimwili na kijamii, kuanzia ndani ya jumuiya zao wenyewe na kisha pole pole wakipanua jitihada zao hadi kukumbatia jamii pana zaidi.

Katika kipindi cha `Abdu'l-Bahá, baadhi ya jumuiya za Kibahá'í huko Iran, pamoja na zingine chache katika nchi jirani, zilikuwa zimefika kwenye kiwango na kufikia hali iliyoziwezesha kufuatilia jitihada zenye mpangilio kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi. `Abdu'l-Bahá alifanya kazi bila kuchoka na marafiki ili kuongoza na kukuza maendeleo yao. Kwa mfano, Yeye aliwahamasisha waumini huko Iran kuanzisha shule za wasichana hali kadhalika za wavulana, kutoka sekta zote za jamii, ambazo zingetoa mafunzo ya tabia njema hali kadhalika sanaa na sayansi. Aliwatuma waumini kutoka Magharibi ili kusaidia katika kazi hii ya maendeleo. Kwenye vijiji vya Kibahá'í vya karibu na 'Adasíyyih na mbali sana huko Daidanaw Yeye alitoa mwongozo kwa vyote viwili usitawi wa kiroho na wa kimwili wa jumuiya hizi. Alielekeza kwamba taasisi tegemezi zianzishwe kwa ajili ya elimu na huduma zingine za kijamii karibu na Mashriqu'l-Adhkár huko 'Ishqábád. Kwa uhamasishaji Wake, shule zilianzishwa huko Misri na Caucasus. Baada ya kifo Chake, Shoghi Effendi alitoa mwongozo wa kupanua juhudi hizi. Shughuli za kukuza afya, kusoma na kuandika, na elimu ya wanawake na wasichana zilienea kwenye jumuiya nzima ya Iran. Zikichochewa na msukumo wa awali ambao `Abdu'l-Bahá alikuwa ameutoa, shule ziliendelea kufunguliwa katika miji na vijiji kote katika nchi hiyo. Shule hizi zilishamiri kwa muda, zikichangia kwenye usasishaji wa taifa hilo, hadi 1934 ambapo zililazimishwa kufungwa na serikali.

Kwingineko, hata hivyo, Shoghi Effendi aliwashauri marafiki kuelekeza rasilimali watu na rasilimali fedha chache zilizokuwepo kwenye ufundishaji na uinuaji wa Utaratibu wa Utawala. Barua iliyoandikwa kwa niaba yake ilieleza kwamba "michango yetu kwa Imani ndiyo njia ya uhakika zaidi ya uinuaji mara moja na kwa wakati wote wa mzigo wa njaa na taabu kutoka kwa wanadamu, kwa kuwa ni kupitia tu mfumo wa Bahá'u'lláh—mtakatifu kwa asili—kwamba ulimwengu unaweza kurudishiwa tena ahueni yake". Wengine "hawawezi kuchangia kwenye kazi yetu au kuifanya kwa ajili yetu", barua iliendelea, "kwa hiyo, kwa kweli, wajibu wetu wa kwanza ni kusaidia kazi yetu wenyewe ya ufundishaji, kwani hii ndiyo italeta uponyaji wa mataifa". Wakati watu binafsi walipata nafasi binafsi ambazo kwazo wangeweza kuchangia kwenye maendeleo ya kimwili na kijamii, kwa jumla Wabahá'í walielekeza rasilimali zao kwenye ukuaji na ujenzi wa jumuiya zao. Katika miaka ya mwanzoni kufuatia uchaguzi wa Nyumba ya Haki, miongozo iliendelea kwa muda kwa mwelekeo huo huo. Kwa hiyo, ingawa dhana ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi imo katika mafundisho ya Bahá'u'lláh, kwa sababu ya hali za Imani katika kipindi chote cha utumishi wa Mlinzi na miaka iliyofuatia, ilikuwa imuhali kwa sehemu kubwa kabisa ya ulimwengu wa Kibahá'í kufanya shughuli za maendeleo.

Mnamo 1983, baada ya miongo kadhaa ya jitihada isiyolegea katika uga wa ufundishaji na kama matokeo ya ukuaji mkubwa katika nchi nyingi kote ulimwenguni, jumuiya ya Jina Kuu ilikuwa imefikia hatua ambayo kwayo kazi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi ingepaswa—kwa kweli, kuwa—imeingizwa katika shughuli zake za kila siku. Marafiki walihimizwa kujitahidi, kupitia

utumiaji wao wa kanuni za kiroho, unyofu wa mwenendo, na utumiaji wa ustadi wa ushauriano, kujiinua wenyewe na hivyo kuchukua wajibu kama mawakala wa maendeleo yao wenyewe. Ofisi ya Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi ilianzishwa kwenye Makao Makuu ya Ulimwengu ili kuisaidia Nyumba ya Haki kukuza na kuratibu shughuli za marafiki katika uga huu kote ulimwenguni, na baada ya muda ilibadilika ili kuwezesha mchakato wa kiulimwengu wa ujifunzaji kuhusu maendeleo. Waumini binfasi waliinuka kuanzisha shughuli mbalimbali zikikumbatia si tu Wabahá'í bali pia jumuiya pana zaidi.

Ndani ya muongo mmoja, mamia ya shughuli za maendeleo zilikuwa zimeanzishwa ulimwenguni, zikishughulikia masuala mbalimbali kama vile maendeleo ya wanawake, elimu, afya, mawasiliano ya umma, kilimo, shughuli za kiuchumi, na mazingira. Shughuli hizi zilipangiliwa sambamba kwenye wigo wa utata. Shughuli rahisi za kawaida za muda mfupi katika vijiji na miji ziliandaliwa katika kushughulikia matatizo na changamoto maalum zilizoyakabili maeneo hayo. Miradi endelevu, kama vile shule na kliniki, zilianzishwa ili kukidhi mahitaji ya kijamii kwa kipindi cha muda mrefu, aghalabu sambamba na miundo ya kimashirika ili kuhakikisha uwezekano wao wa kujitegemea na ufanisi. Na hatimaye, kufikia 1996, mashirika machache yenye uvuvio wa Kibahái yenye miundo ya programu tata kiasi yalianzishwa na watu binafsi ili kujifunza kufuatilia kiutaratibu mbinu yenye mfungamano ya maendeleo, ndani ya idadi ya watu, ambayo ingesababisha athari muhimu katika eneo hilo. Katika jitihada zote hizi, marafiki walitafuta kutumia kanuni za kiroho kwenye matatizo ya kiutendaji.

Kadiri mawakala wenye uvuvio wa Kibahái hali kadhalika na mawakala walio chini ya mamlaka ya moja kwa moja ya asasi za Kibahá'í walivyoanza kujitokeza katika nchi moja hadi nyingine, athari ya juhudi zao ndani ya jumuiya na ya jamii pana ikaendelea kuwa wazi zaidi, wakidhihirisha mfungamano wenye nguvu kati ya vipengele vya kimwili na vya kiroho vya maisha. Maendeleo hayakutokea tu katika vitendo, bali pia katika ngazi ya fikra. Marafiki walikuja kuelewa seti ya dhana za kimsingi: ulimwengu haujagawanywa katika vipengele vya walioendelea na wasioendelea—wote wanahitaji mabadiliko na mazingira yanayowapatia hali za kiroho, kijamii na kimwili ambavyo ni vya muhimu kwa ajili ya ulinzi na usitawi wao. Maendeleo siyo mchakato unaofanywa na watu fulani kwa niaba ya wengine; bali, watu wenyewe, popote waishipo, ndio wahusika wakuu wa maendeleo yao wenyewe. Kupata maarifa na kushiriki katika uzalishaji, matumizi, na usambazaji wake kupo katika kiini cha jitihada hii. Jitihada huanza kidogo kidogo na hukua katika utata kadri tajiriba inavyojikusanya. Programu ambazo ufanisi wake umeonekana katika eneo moja zinaweza kuanzishwa kwa mpangilio katika maeneo mengine. Kadiri kanuni na dhana hizi zitumikavyo ndani ya mazingira mahsusi, marafiki wanakuwa wenye ujuzi zaidi wa kuchambua hali zao za kijamii, wakichota umaizi kutoka Maandiko na kutoka nyanja anuai husika za maarifa, na kuanzisha shughuli ambazo zimejumuishwa kikamilifu pamoja na kazi ya ujenzi wa jumiuya.

Hadi kufikia 2018, ueneaji mkubwa na utata ulioongezeka wa jitihada za Kibahá'í za maendeleo kote ulimwenguni ulikuwa umechochea uanzishwaji wa asasi mpya katika nchi takatifu—Shirika la Maendeleo ya Kibahá'í la Kimataifa. Asasi hii ya kiulimwengu ilijitwalia, na hupanua zaidi, kazi na mamlaka iliyofanywa hapo awali na Ofisi ya Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi, ikiimarisha jitihada ya hatua za kijamii za watu binafsi, jumuiya, asasi, na mawakala kila mahali.

Kama ilivyokuwa kwa Ofisi iliyoitangulia, kusudi lake la msingi ni kuwezesha mchakato wa kiulimwengu wa ujifunzaji kuhusu maendeleo unaokunjuka katika ulimwengu wa Kibahá'í, kwa kukuza na kusaidia utendaji na tafakari, ukusanyaji na upangiliaji wa tajiriba, uundaji wa dhana, na mafunzo—yote yakifanywa kulingana na mafundisho ya Imani. Hatimaye, inatafuta kukuza kipekee mbinu za Kibahá'í juu ya maendeleo.

Sambamba na ukunjukaji wenye mpangilio wa michakato ya upanuzi na uimarishaji na ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi, eneo lingine kubwa la utendaji liliibuka: ushiriki mkubwa katika mijadala iliyoenea ya kijamii. Kwa idadi iongezekayo ya mazingira ya kijamii ambapo majadiliano kuhusu matatizo ya kibinadamu hutokea, Wabahá'í hutafuta kushiriki umaizi stahiki ukichotwa kutoka bahari ya Ufunuo wa Bahá'u'lláh. Ni Bahá'u'lláh Mwenyewe ndiye Ambaye tangu mwanzo alitangaza moja kwa moja tiba Yake iponyayo kwa viongozi wa ulimwengu na aliwasihi binadamu wote kuifuata. Licha ya kushindwa kwa wafalme na watawala kuitikia kwa uthabiti kwenye asili takatifu ya dai Lake, Yeye aliwasihi kutumia kanuni zake kwa ajili ya kusimamisha amani ya ulimwengu: "Sasa kwa kuwa mmeikataa Amani Kuu Kabisa, shikilieni kwa uthabiti katika hii, Amani Ndogo, ili huenda mkaweza, kwa kiasi fulani, kuboresha hali yenu wenyewe na ile ya wategemezi wenu." 'Abdu'l-Bahá, katika Maandiko kama vile Nyaraka kwenda Hague, na hususan katika mazungumzo yaliyotolewa wakati wa safari zake kwenda Magharibi, bila kukoma alitangaza Mafundisho ya Baba Yake kwa wenye nguvu na raia wanaopambana na matatizo mengi yanayoikumba jamii ya mwanadamu.

Mwanzoni mwa utumishi wake, Shoghi Effendi, akiwa na ufahamu juu ya umuhimu wa lazima kuwafahamisha watu na viongozi wa ulimwengu umaizi na hekima zilizomo kwenye mafundisho ya Kibahá'í, alikuza mipango kwa ajili ya kusudi hili. Hii ilijumuisha, pamoja na mingine, ufunguzi wa ofisi ya habari za Kibahá'í huko Geneva 1925, uchapishaji wa vitabu 'Ulimwengu wa Kibahá'í', na mwito kwa Wabahá'í wenye maarifa kuhusianisha Mafundisho na fikra za kisasa kuhusiana na matatizo mengi ya haraka yanayoukabili ulimwengu. Baada ya kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa, Jumuiya ya Kibahá'í ya Kimataifa ilianzishwa 1948 kama shirika lisilo la kiserikali likiiwakilisha jumuiya za Kibahá'í kote ulimwenguni na likazidi kujishughulisha na vipengele vya kazi ya chombo hicho cha kimataifa. Hii ilifungua sura mpya katika kuendeleza uhusiano wa Imani na serikali, asasi za kiulimwengu, na wakala wa asasi za kiraia katika uwanja wa kimataifa. Wakati kamwe hakuruhusu eneo hili la jitihada kutotilia maanani umuhimu wa kwanza wa kazi ya ufundishaji, Mlinzi aliwahamasisha marafiki kuifahamisha jumuiya pana athari za mafundisho ya Bahá'u'lláh. "Sambamba na mchakato huu wa uimarishaji wa mfumo wa Utaratibu wa Kiutawala na upanuzi wa msingi wake," yeye aliiandikia jumuiya moja ya kitaifa, "jaribio thabiti lazima lifanywe" kwa ajili ya uanzishwaji wa mawasiliano ya karibu zaidi na, miongoni mwa zingine, "viongozi wenye fikra wa umma". Akisisitiza ushirikiano badala ya ushirikishwaji, na akiwasihi waumini kubakia bila mawaa kwa ushiriki wowote katika masuala ya kisiasa, aliwahamasisha kujihusisha na mashirika yenye mwelekeo sawa yanayojihusisha na masuala ya kijamii na kuyafahamisha shabaha na makusudi ya Imani na asili ya mafundisho yake juu ya masuala kama vile uanzishwaji wa amani ya ulimwengu.

Baada ya kuanzishwa kwa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, mchakato huu wa kushiriki katika mijadala ya kijamii ulipanuliwa zaidi. Katika nyakati muafaka, Nyumba ya Haki ilipanga kueneza kwa mpana kanuni za Imani, kama katika ujumbe wake kwa watu wa ulimwengu, "Ahadi ya Amani ya Ulimwengu". Jumuiya ya Kibahá'i ya Kimataifa iliimarisha nafasi yake kwenye Umoja wa Mataifa, hatimaye ikajipatia ushirikiano rasmi zaidi na mawakala mbalimbali wa Umoja wa Mataifa kwenye miaka ya 1970. Ilichapisha taarifa juu ya masuala ya ulimwengu na kutengeneza nafasi ya kipekee kwa ajili ya ushirikiano na serikali hali kadhalika mashirika yasiyo ya kiserikali. Ikitambuliwa na wale inaoshirikiana nao kama wasiokuwa na ajenda yenye maslahi-binafsi lakini ikifanya kazi kwa ajili ya usitawi wa watu wote, ilichukua nafasi muhimu katika makongamano mbalimbali ya kimataifa, likiwemo kongamano la Mazingira na Maendeleo Endelevu kule Rio de Janeiro, Kongamano la Ulimwengu la Wanawake huko Beijing, Mkutano Mkuu wa Ulimwengu kwa ajili ya Maendeleo ya Kijamii huko Copenhagen, na Jukwaa la Milenia huko New York. Kufuatia Mapinduzi ya Iran na kuanza upya kwa mateso ya Wabahá'i huko Iran, jumuiya kadhaa za kitaifa zilisukumwa kuingia katika mabadilishano ya karibu zaidi ya mawazo pamoja na asasi na mawakala mbalimbali wa kitaifa na kimataifa. Matokeo yake zilianzisha ofisi za kitaifa za mambo ya nje ili kuimarisha jitihada kwenye ngazi ya Kimataifa za kulinda Imani.

Kadiri karne ya ishirini na moja ilivyoanza, maendeleo ya kimfumo ya Hoja yalitengeneza mazingira kwa ajili ya ushiriki wenye utaratibu zaidi katika mijadala ya kijamii. Tovuti za Kibahá'í za kimataifa na kitaifa kwa kasi kubwa ziliendeleza uwasilishaji wa Mafundisho kwa mlolongo mpana wa mada. Taasisi ya Masomo kwa ajili ya Usitawi wa Ulimwengu ilianzishwa ili kufanya utafiti juu ya athari za mafundisho ya Bahá'u'lláh kwenye masuala ya shinikizi ya kijamii; baada ya muda pia ilianzisha mfululizo wa semina za kujenga uelewa na kukuza uwezo miongoni mwa wanafunzi wa Kibahá'i wa vyuo vikuu. Kazi ya Jumuiya ya Kibahá'i ya Kimataifa, awali ikijikita huko New York na Geneva, ilipanuliwa hadi kwenye vituo vya kanda huko Addis Ababa, Brusels, na Jarkata. Kwenye ngazi ya kitaifa, ofisi za mambo ya nje zilijifunza zaidi jinsi ya kushiriki katika mijadala maalum ya kitaifa kwa namna iliyopangiliwa kwa niaba ya jumuiya zao husika. Miongoni mwa mada zilizozungumziwa kwa kina kwenye mataifa mbalimbali zilikuwa juu ya maendeleo ya wanawake, wajibu wa dini katika jamii, uwezeshaji kiroho na kimaadili wa vijana, ukuzaji wa haki, uimarishaji wa mshikamano wa kijamii. Leo, mchakato wa kiulimwengu wa ujifunzaji kutokana na tajiriba ya kuchangia kwenye mijadala hii ya kitaifa unawezeshwa na Ofisi ya Mijadala ya Umma kwenye Makao Makuu ya Kibahá'i ya Ulimwengu. Na kwenye ngazi ya chini kabisa katika ujirani na vijiji, na katika taaluma zao na katika nafasi zingine za kijamii ambamo wanashiriki kama watu binafsi, marafiki wanajifunza kutoa dhana kutoka kwenye Maandiko ya Kibahá'i kama mchango kwenye mageuzi ya kifikira na utendaji miongoni mwa wananchi wenzao ambayo ni ya lazima katika kuleta mabadiliko chanya.

Ujihusishaji kwenye ngazi zote hizi za kijamii unakuwa wenye kushinikiza zaidi kadiri mchakato wa uchangukaji wa utaratibu wa ulimwengu wa zamani unavyozidishwa na mjadala unavyodunishwa na kukingana zaidi, ukisababisha kuzuka tena kwa migogoro miongoni mwa vikundi na fikira shindani zinazoigawa jamii ya mwandamu. Katika kuendana na uelewa wao kwamba mabadiliko yaliyotazamiwa na Bahá'u'lláh huhitaji ushiriki wa kila mmoja, Wabahá'i wanatafuta kufanya kazi na watu wengi binafsi wenye huruma na mashirika yanayofuata malengo ya pamoja. Katika jitihada za kiushirikiano kama hizo, marafiki wanashiriki umaizi kutoka

mafundisho ya Bahá'u'lláh hali kadhalika masomo ya kivitendo yaliyopatikana katika jitihada zao za ujenzi wa jumuiya, wakati huo huo wakijifunza kutokana na tajiriba ya wenzao wanaoshirikiana nao. Katika kufanya kazi na watu binafsi, jumuiya, na mashirika, yote mawili ya kiraia na ya kiserikali, marafiki wanadumisha ufahamu kwamba majadiliano juu ya masuala mengi ya kijamii yanaweza kuwa yenye kuleta ubishi au kuingizwa kwenye matarajio ya kisiasa. Katika mazingira yote ambamo Wabahá'i hujihusisha kwa kina zaidi na jumuiya pana, wanatafuta kukuza maelewano na umoja wa fikra, na kuendeleza ushirikiano na utafutaji wa pamoja wa suluhu kwa matatizo shinikizi ya binadamu. Kwao, njia ambayo kwayo mwisho hufikiwa ni muhimu kama ulivyo mwisho wenyewe.

Kadiri mchakato wa kujihusisha daima zaidi na maisha ya jamii pana ulivyojikita mizizi katika jumuiya za Kibahá'í kote ulimwenguni, awali ulikunjuka bega kwa bega na kazi ya ufundishaji na maendeleo ya utawala. Katika miongo ya hivi karibuni, hata hivyo, jitihada kwa ajili ya shughuli za kijamii na ushiriki katika mijadala ya kijamii zimefanikisha mfungamano mkubwa na zile za upanuzi na uimarishaji kwani marafiki wameendelea kutumia vipengele vya muundo wa dhana kwa ajili ya utendaji wa Mipango ya ulimwengu. Kadiri marafiki wanavyojibidiisha katika klasta zao, bila kuzuilika wanajiingiza katika maisha ya jamii inayowazunguka, na mchakato wa ujifunzaji unaosukuma jitihada za ukuaji na ujenzi wa jumuiya unapanuliwa hadi kwenye mlolongo upanukao wa shughuli. Maisha ya jumuiya yanaendelea kupambanuliwa kwa uchangiaji wake kwenye maendeleo ya kimwili, kijamii na kiroho kadiri marafiki wanavyokuza uwezo wao wa kuelewa hali za jamii inayowazunguka, wanatengeneza nafasi ambamo wanachunguza dhana kutoka Ufunuo wa Bahá'u'lláh na kutoka nyanja husika za maarifa ya binadamu, wanaleta umaizi unaoathiri matatizo ya kiutendaji, na kujenga uwezo miongoni mwa waumini na ndani ya jumuiya pana zaidi. Kama matokeo ya mfungamano huu unaokua kwenye maeneo mbalimbali ya jitihada, shughuli nyingi za kimsingi kwenye ngazi ya chini kabisa kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi ziliongezeka kutoka mamia kadhaa miaka ya 1990 hadi maelfu kadhaa miaka ya 2000, na hadi kufikia makumi ya maelfu mnamo miaka ya 2021. Ushiriki wa Wabahá'i katika mijadala ya kijamii umefikiwa na mwitikio mkubwa wa kukubalika katika mazingira yasiyohesabika, kutoka ujirani hadi mataifa, kadiri jamii ya mwanadamu iliyochanganyikiwa na kugawanyika kwa matatizo mengi yatokanayo na utendaji wa nguvu za uchangukaji, inavyotafuta kwa shauku umaizi mpya. Kwenye ngazi zote za kijamii, viongozi wenye fikra wanaendelea kuihusisha jumuiya ya Kibahá'i na mawazo na mbinu mpya zihitajikazo kabisa na ulimwengu usio na umoja na usiofanya kazi daima. Nguvu ya Imani ya ujenzi wa jamii, iliyomo kwa kiasi kikubwa katika hali ya isiyodhihirika mwanzoni mwa karne ya kwanza ya Zama za Ujenzi, sasa inaendelea kuonekana nchi hadi nchi. Uachiliaji wa nguvu hii ya ujenzi wa jamii itokanayo na ufahamivu mpya na uwezo mpya wa ujifunzaji miongoni mwa watu binafsi, jumuiya, na asasi kote ulimwenguni imekusudiwa kuwa alama mahsusi ya hatua ya sasa na kadhaa zinazofuata katika ukunjukaji wa Mpango Mtakatifu.

Maendeleo ya Makao Makuu ya Kibahá'í ya Ulimwengu

Sambamba na ukuaji wa Imani na ukunjukaji wa utawala, maendeleo yenye umuhimu sawa yalitokea kwenye Makao Makuu ya Kibahá'í ya Ulimwengu katika karne ya kwanza ya Zama za Ujenzi, iliyoanzishwa kwa msukumo wa Hati nyingine, Waraka wa Bahá'u'lláh wa Carmel. Tayari

imekwishatajwa kuhusu mwingiliano kati ya michakato inayohusiana na Hati hizo tatu, ikijumuisha utokeaji wa asasi na mawakala wa Makao Makuu ya Kibahá'í ya Ulimwengu. Kwa maelezo haya sasa baadhi ya tafakari inaweza kuongezwa juu ya maendeleo ya makao yake ya kiroho.

Wakati nyayo za Bahá'u'lláh zilipogusa ufuko wa 'Akká, sura ya upeo wa Utumishi Wake ilianza. Bwana wa Majeshi alidhihirishwa katika Nchi takatifu. Kuwasili kwake kulitabiriwa kupitia ndimi za manabii maelefu ya miaka kabla. Utimilizo wa utabiri huo, hata hivyo, haukuwa matokeo ya hiari Yake Mwenyewe, bali ulishurutishwa na mateso Yake mikononi mwa adui Zake wa wazi wazi, ukiishia na uhamisho Wake. "Tulipowasili," Yeye alisema katika Waraka mmojawapo, "tulikaribishwa kwa beramu ya mwanga, ndipo Sauti ya Roho ikapiga kelele ikisema: 'Hivi punde wote waishio duniani wataandikishwa chini ya beramu hizi'". Nguvu ya kiroho ya nchi ile iliongezeka kupita kiasi kwa uwepo Wake na maziko ya Mabaki Yake Matakatifu na, baadaye kidogo, yale ya Mtangulizi Wake, Yeye Mwenyewe Mdhihirishaji wa Mungu. Sasa ni mahali ambako kila moyo wa Mbahai huelekezwa, kituo lengwa cha ibada zao, lengo la kila hujaji mwenye shauku. Maeneo Matakatifu ya Kibahá'í huwakaribisha watu wa Nchi Takatifu, na kwa hakika watu wa kila nchi. Ni amana yenye thamani inayolindwa kwa wanadamu wote.

Hata hivyo, umiliki wa Wabahá'í kwenye makao makuu ya kiroho ya Imani yao mwishoni mwa Zama za Kishujaa na kwa miaka mingi baadaye haukuwa kamili. Ilikuwa vigumu jinsi gani, wakati fulani, kwa 'Abdu'l-Bahá hata kusali kwenye mahali pa mapumziko pa Baba Yake. Hali yake ilikuwa mbaya kiasi gani, akishtakiwa kwa uwongo kwa uchochezi kwa kujenga jengo ambamo, kwa amri ya Bahá'u'llah, mabaki ya kimwili ya Báb yalilazwa baada ya safari ndefu kutoka mahali pa kifo Chake cha kishahidi. Hali ya hatari na isiyo salama ya Makao Makuu ya Ulimwengu iliendelea hadi kwenye utumishi wa Mlinzi, kama ilivyodhihirika wakati funguo za Kaburi Takatifu la Bahá'u'llah zilipoporwa na Wavunja Agano muda mfupi baada ya kuchukua majukumu yake. Hivyo, miongoni mwa majukumu ya kwanza na muhimu zaidi ya Shoghi Effendi, aliyoyatekeleza katika kipindi chote cha utumishi wake, yalikuwa ulinzi na uhifadhi, upanuzi na urembeshaji wa Makaburi Matakatifu pacha na Maeneo mengine Matakatifu. Ili kufanikisha lengo hili, ilimbidi aongoze kipindi cha mabadiliko yenye msukosuko kwenye Nchi Takatifu—yakijumuisha mvurugiko wa kiuchumi wa dunia, vita, mageuzi ya mara kwa mara wa kisiasa, na ukosefu wa utangamano wa kijamii—huku akishikilia, kama ilivyokuwa kwa `Abdu`l-Bahá kabla yake, kanuni za zisizobadilika za Kibahá`i za ushirika na watu wote na heshima kwa mamlaka iliyowekwa ya kiserikali. Wakati fulani, hata ilimbidi atafakari kuhamisha mabaki ya Bahá`u`lláh hadi kwenye mazingira yanayofaa kwenye Mlima Carmel ili kuhakikisha ulinzi wake. Na kwa uthabiti alibaki Haifa wakati wa misukosuko hiyo na mizozo, kama vile alivyolielekeza kundi dogo la waumini wa eneo hilo kutawanyika sehemu zingine za dunia. Wajibu huu mgumu lakini uliofuatiliwa bila kuchoka uliendelea hadi siku zake za mwisho, wakati Kaburi Takatifu la Bahá'u'lláh hatimaye lilipotambuliwa kama Mahali Patakatifu pa Kibahá'í na mamlaka za kiraia, na ulimwengu wa Kibahá'í hatimaye ukawa huru kuhifadhi na kurembesha mahali pake patakatifu kabisa.

Wakati wa jitihada zake za kupata, kurejesha, na kulinda Maeneo Matakatifu, Mlinzi alipanua kwa kiasi kikubwa mali zinazozunguka Kaburi Takatifu na Jumba la Bahjí na alianzisha kile ambacho hatimaye kingekuwa bustani kubwa rasmi. Kwenye Mlima wa Mungu, alilikamilisha Kaburi Takatifu la Báb liliocheleweshwa kwa muda mrefu, lililoanzishwa na ‘Abdu’l-Bahá, akiongeza vyumba vitatu vya ziada, akaunda njia tao yake, akainua kuba yake la dhahabu, na kulizunguka kwa bustani za chanikiwiti. Alifuatilia "tao lililoenea sana ambapo kuzunguka kwalo majengo ya Utaratibu wa Kiutawala wa  Kibahá'í wa Ulimwengu" yangejengwa; akiinua kwenye ncha moja ya tao hilo jengo lake la kwanza, Jengo la Makavazi la Kimataifa; na aliweka katikati yake, mahali pa kupumzika pa Jani Takatifu Kabisa, kaka yake, na mama yao. Kazi za Mlinzi kwa ajili ya maendeleo ya Makao Makuu ya Ulimwengu ziliendelezwa chini ya uongozi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Ardhi ya ziada na Mahali Patakatifu palipatikana na kurembeshwa, majengo kwenye Tao hilo yaliinuliwa, na ngazi zilipanuliwa kutoka chini hadi juu ya Mlima Carmel, kama ilivyotazamiwa na ‘Abdu’l-Bahá hapo awali na kuanzishwa na Mlinzi. Kabla ya kumalizika kwa karne ya kwanza ya Zama za Ujenzi, eneo lilikuwa katika ujirani wa Kaburi la Báb liliongezwa hadi zaidi ya mita za mraba 170,000, huku mfululizo wa ubadilishanaji wa ardhi na ununuzi ukipanua eneo hilo lililokuwa karibu na Kaburi Takatifu la Baha'u’llah kutoka mita za mraba 4,000 hivi hadi zaidi ya 450,000. Na mnamo 2019 ujenzi wa Kaburi litakalofaa kuwa kama mahali pa mapumuziko ya mwisho ya 'Abdu'l-Bahá ulianza huko 'Akka, karibu na Bustani ya Riḍván.

Katika kipindi cha karne hiyo, kasi ya maendeleo ya makao makuu ya utawala ya Kibahá’í pia ilichapuzwa. Kwa miaka mingi, mapema katika utumishi wake, Mlinzi alitamani sana msaada wa wasaidizi wenye uwezo, lakini ulimwengu wa Kibahá’í wakati huo ulikuwa mdogo mno kuweza kutoa msaada uliohitajika. Kadiri jumuiya ilivyokua, hata hivyo, Nyumba ya Haki iliweza kuendelea kunufaika kutokana na mtiririko endelevu wa watu walijitolea kuanzisha idara na mawakala wa muhimu sana kwa Imani ikuayo kwa kasi, kuhudumia mahitaji kwenye Makao Makuu ya Ulimwengu hali kadhalika kwa jumuiya zilizoongezeka kote duniani. Maswali na ushauri, umaizi na miongozo, wageni na mahujaji sasa wanatiririka bila kukoma kati ya sehemu zote za sayari na katikati ya ulimwengu wa Kibahá’í. Mnamo 1987, baada ya miongo kadhaa ya mabadiliko na mashaka, juhudi za subira zilizoanzishwa mapema zadi na Shoghi Effendi kuanzisha uhusiano mzuri na mamlaka za kiraia huko Israel ilifikia kilele cha utambuzi rasmi wa hadhi ya Makao Makuu ya Kibahai ya Ulimwengu kama kituo cha kiroho na cha kiutawala cha Jumuiya ya Kibahá'í ulimwenguni, kinachofanya kazi chini ya uangalizi wa Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.

Kama vile uhusiano miongoni mwa watu binafsi, jumuiya, na asasi umekuwa ukibadilika baada ya muda, ukijengwa juu ya mafanikio ya awali na kuinuka kukabiliana na changamoto mpya, hivyo ndivyo inavyoweza kusemwa kuhusu Makao Makuu ya Kibahá’í na uhusiano wake na Wabahá'í kote ulimwenguni. Uhusiano wa karibu na usiotenganishika wa makao makuu ya kiroho na kiutawala na maendeleo ya ulimwengu wa Kibahá'í ulielezwa katika ujumbe wa 24 Mei 2001 tuliowaandikia waumini waliokusanyika kwa ajili ya matukio ya yaliyoashiria ukamilikaji wa miradi juu ya Mlima Carmel: "Majengo ya kifahari ambayo sasa yamesimama kando ya Tao lililochorwa na Shoghi Effendi kwa ajili ya hayo kwenye mteremko wa Mlima wa Mungu, pamoja na mteremko wa ajabu wa ngazi zenye bustani zinazokumbatia Kaburi la Báb, ni kielelezo cha nje cha nguvu kubwa ihuishayo Hoja tunayoitumia. Yainatoa ushahidi usioathiriwa na wakati kwenye

ukweli kwamba wafuasi wa Baha'u'lláh wamefanikiwa kuweka misingi ya jumuiya ya kiulimwengu inayovuka tofauti zote zinazoigawanya mbari ya binadamu, na wameanzisha asasi kuu za Utaratibu wa Kiutawala wa kipekee na usioshambulika unaobumba maisha ya jumuiya hii. Katika mabadiliko yaliyotokea kwenye Mlima Carmel, Hoja ya Kibaha'i huibuka kama uhalisia ulio wazi na wa kuvutia sana kwenye jukwaa la kimataifa, kama kitovu kikuu cha nguvu ambazo, kwa wakati mzuri wa Mungu, zitaleta ujenzi mpya wa jamii, na kama chanzo cha ajabu cha uhuisho wa kiroho kwa wote wanaoigeukia."

Matarajio

Majuma machache kabla ya kufariki, `Abdu`l-Bahá alikuwa nyumbani kwake na mmoja wa marafiki Zake. "Nifuate" alisema: "ili tuweze kufurahia kwa pamoja uzuri wa bustani". Kisha alitoa wazo: "Tazama kile ambacho moyo wa ibada waweza kukitimiza! Eneo hili lenye kushamiri, miaka michache iliyopita, halikuwa chochote ila rundo la mawe, na sasa linasitawi kwa mimea na maua. Shauku yangu ni kwamba nikishaondoka, wapendwa waweze kuinuka kuitumikia Hoja takatifu, na Mungu aridhie, iwe hivyo." "Punde si punde" Yeye aliahidi: watajitokeza wale "ambao wataleta uhai ulimwenguni".

Marafiki wapendwa sana! Mwishoni mwa Karne ya Kwanza ya Zama za Ujenzi, ulimwengu wa Kibahá'i unajikuta wenyewe umejaliwa na uwezo na rasilimali zilizodhaniwa kwa ufinyu tu wakati wa kufariki kwa `Abdu`l-Bahá. Kizazi hadi kizazi kimejitahidi, na leo umati umeinuliwa ambao umesambaa kote ulimwenguni—roho zilizowekwa wakfu ambazo kwa pamoja zinajenga Utaratibu wa Kiutawala wa Imani, zikipanua ufikaji wa maisha yake ya jumuiya, zikiimarisha ushiriki wake na jamii, na kuendeleza makao yake ya kiroho na ya kiutawala.

Mapitio haya mafupi ya miaka mia moja yameonesha namna jumuiya ya Kibahá'í, katika kujitahidi kutekeleza kimpangilio Hati tatu Takatifu, imekuwa uumbaji mpya kama ilivyotazamiwa na `Abdul-Bahá. Kama vile mwanadamu hupitia hatua mbali mbali za ukuaji wa kimwili na kiakili na maendeleo hadi kufikia utu uzima, vivyo hivyo pia jumuiya ya Kibaha'i hukua taratibu, kwa ukubwa na muundo, hali kadhalika katika uelewa na muono, ikikumbatia majukumu na kuimarisha uhusiano miongoni mwa watu binafsi, jumuiya na asasi. Kwa kipindi cha karne hiyo, kwenye mazingira ya asili hali kadhalika katika ngazi ya kiulimwengu, mfululizo wa maendeleo uliopitiwa na jumuiya ya Kibaha'i umeiwezesha kufuatilia hatua za makusudi kwenye jitihada mbalimbali na pana zaidi.

Wakati Zama za Kishujaa zilipokaribia mwishoni, jumuiya ilikabiliana na masuala ya kimsingi kuhusu jinsi ya kupangilia masuala yake ya kiutawala, ili kuitikia kwenye mahitaji ya Mpango Mtakatifu. Mlinzi aliwaongoza marafiki katika kujifunza namna ya kushughulikia masuala hayo ya awali, mchakato uliofikia kilele katika mipangalio michanga ya kimataifa iliyokuwepo wakati wa kufariki kwake. Uwezo uliojengwa katika kipindi hicho uliuwezesha ulimwengu wa Kibaha'i kuchukua masuala mengi mapya juu ya namna ya kutekeleza kazi ya Imani kwa kiwango kikubwa zaidi cha mapana na utata chini ya maelekezo ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu. Kisha, bado tena, baada ya kufanya maendeleo halisi kwa miongo mingi, hata masuala zaidi juu ya fursa ambazo bado zilikuwa kubwa zaidi kuhusu mwelekeo wa baadaye Hoja ziliibuka kabla ya kuanza kwa Mpango wa Miaka Minne, ambao uliweka changamoto mpya kwa ajili ya kipindi cha ziada

cha maendeleo, ukisisitiza kwenye kufanikisha maendeleo ya maana katika mchakato wa uingiaji kwa makundi katika sehemu zote za ulimwengu. Ni uwezo huu huu unaoongezeka wa kutatua masuala tata na kisha kuchukua hata masuala tata zaidi unaopambanua mchakato wa ujifunzaji ambao husukuma maendeleo ya Imani. Hivyo, ni dhahiri kwamba kwa kila hatua ifuatayo katika ukunjukaji wake wa taratibu, ulimwengu wa Kibahá'i hukuza nguvu mpya na uwezo mpya ambao huwezesha kuchukua changamoto kubwa zaidi, kadiri unavyokazana kufanikisha kusudi la Bahá`u`lláh kwa binadamu. Na itaendelea kuwa hivyo, licha ya mabadiliko na nasibu za ulimwengu, kupitia hali ya hatari na ushindi, na mabadiliko mengi yasiyotarajiwa, kupitia hatua zisizohesabika za Zama za Ujenzi na za Dhahabu hadi mwisho wa Kipindi hiki Kitakatifu.

Hadi kufikia miaka ya mwisho ya Karne ya Kwanza ya Zama za Ujenzi, mfumo wa pamoja wa kiutendaji ulikuwa umekwishaibuka ambao umekuwa muhimu sana kwa kazi ya jumuiya, na ambao unafahamisha fikra na kutoa muundo kwa shughuli zilizo tata zaidi na zaidi na zenye kufaa. Mfumo huu unaendelea kubadilika kupitia mkusanyiko wa tajiriba na miongozo wa Nyumba ya Haki. Vipengele muhimu vya mfumo huu ni kweli za kiroho na kanuni za kimsingi za Ufunuo huu. Vipengele vingine ambavyo pia huchangia kwenye fikra na utendaji huhusisha maadili, mitazamo, dhana na mbinu. Bado vingine hujumuisha uelewa wa ulimwengu wa kimwili na ule wa kijamii kupitia umaizi kutoka matawi mbali mbali ya maarifa. Ndani ya mfumo huu uendeleao kubadilika, Wabahá`i wanajifunza namna ya kutafsiri kimpangilio mafundisho ya Bahá`u`lláh katika vitendo ili kufanikisha shabaha Zake za hali ya juu kwa ajili ya uboreshaji wa ulimwengu. Umuhimu wa ongezeko hili la uwezo wa kujifunza na athari zake kwa maendeleo ya binadamu katika hatua ya sasa ya maendeleo ya kijamii hauwezi kukadiriwa kupita kiasi.

Ni kiasi gani ulimwengu wa Kibahá′i umetimiza! Kiasi gani kinabaki kutimizwa! Mpango wa Miaka Tisa huainisha kazi za papo hapo. Miongoni mwa maeneo ya kumakinikia ni uzidishaji na ushadidishaji wa programu za ukuaji katika klasta kote ulimwenguni, na kuongeza mfungamano katika kazi ya ujengzi wa jumuiya, shughuli za kijamii na ushiriki katika mijadala iliyoenea, kupitia juhudi za pamoja za wahusika wakuu watatu wa Mpango. Taasisi ya mafunzo itaimarishwa zaidi na itaendelea kubadilika kama shirika la kielimu linalokuza uwezo kwa ajili ya huduma. Mbegu ambazo inazipanda katika mioyo ya makundi yanayofuatana ya vijana zitalelewa na fursa zingine za kielimu ili kuiwezesha kila roho kuchangia kwenye maendeleo ya kijamii na usitawi. Mjongeo wa vijana utakamilishwa kote ulimwenguni na maendeleo yasiyo na kifani ya wanawake kama washirika kamili katika masuala ya jumuiya. Uwezo wa asasi za Kibahá′i utakuzwa kwenye ngazi zote, kwa umakinifu maalum kwenye uanzishwaji na uendelezwaji wa Mabaraza ya Mahali na kuimarisha ushiriki wao na jamii pana na viongozi wake. Maisha ya kiakili ya jumuiya yatakuzwa ili kuleta umakini na ubayana wa mawazo yanayohitajika kuthibitisha kwa wanadamu wenye mashaka ufaaji wa tiba iponyayo ya mafundisho ya Bahá`u`lláh. Na jitihada zote hizi zitaendelea kupitia mlolongo wa Mipango inayojumuisha changamoto, ikidumu si chini ya kizazi kimoja, ambayo itaupeleka ulimwengu wa Kibahá′i kuvuka kizingiti cha karne yake ya tatu.

Jitihada za dhati za kupata uelewa kamili zaidi wa, na kuishi kulingana na mafundisho ya Bahá`u`lláh. hutokea katika muktadha mkubwa zaidi wa mchakato wa pande mbili wa uchangukaji na uunganishaji ulioelezwa na Shoghi Effendi. Kufikia lengo la mlolongo wa sasa wa Mipango—

uachiliaji kwa viwango viongezekavyo daima vya nguvu ya Imani ya kujenga jamii huitisha uwezo wa kusoma uhalisia wa jamii kadiri unavyoitikia kwenye, na ukibumbwa na michakato hii pacha.

Wingi kupita kiasi wa nguvu za uharibifu na matukio, ikiwemo uharibifu wa mazingira, mabadiliko ya tabia ya nchi, mlipuko wa magonjwa vinavyoenea kote, kuanguka kwa dini na maadili, kupotea kwa maana na utambulisho, mmomonyoko wa dhana za ukweli na utashi, teknolojia isiyozuilika, uzidishaji wa chuki na ugomvi wa mabishano ya kifikra, ufisadi ulioenea, mtikisiko wa kisiasa na kiuchumi, vita na mauaji ya kimbari, zimeacha alama zao katika damu na uchungu kwenye kurasa za historia na kwenye maisha ya mabilioni. Wakati huo huo, mielekeo yenye matumaini inaweza pia kutambuliwa, ambayo huchangia kwenye "fadhaa ya kiulimwengu" ambayo Shoghi Effendi alisema "inakuwa ikitakasa na kubumba upya wanadamu katika matarajio ya Siku ambapo mshikamano wa mbari mzima ya binadamu utakuwa umetambulika na umoja wake kusimikwa". Kuenea kwa moyo wa mshikamano wa ulimwengu, utambuzi mkubwa zaidi wa kutegemeana duniani, kumbatio la hatua ya ushirikiano miongoni mwa watu binafsi na asasi, na shauku inayoongezeka ya haki na amani vinabadilisha kwa kina mahusiano ya binadamu. Na hivyo, mjongeo wa ulimwengu kuelekea muono wa Bahá`u`lláh husonga mbele kwa hatua zisizohesabika za kuchechemea, kwa michupo mikubwa mikubwa ya mara kwa mara, na pamoja na vipindi vya hapa na pale ambapo maendeleo hukwama au hata kurudi nyuma, kadiri wanadamu wanavyotengeneza uhusiano ambao hufanyiza misingi ya ulimwengu wenye umoja na amani.

Nguvu za uharibifu ambazo huutikisa ulimwengu haziiachi jumuiya ya Kibahá′i bila kuguswa. Kwa hakika historia ya kila jumuiya ya Kibahá′i ya kitaifa huwa na alama yake. Kama matokeo, katika maeneo mbalimbali na kwa nyakati tofauti, maendeleo ya jumuiya fulani yalicheleweshwa kutokana na tabia yenye nia mbaya ya kijamii au kuzuiliwa kwa muda, au hata kuzimwa kwa upinzani. Migogoro ya mara kwa mara ya kiuchumi imepunguza rasilimali fedha za Imani ambazo tayari zilikuwa chache, ikizuia miradi ya ukuaji na maendeleo. Madhara ya vita vya ulimwengu yalipoozeshaa, kwa muda, uwezo wa jumuiya nyingi mno kutekeleza mipango kimpangilio. Misukosuko ambayo imebumba upya ramani ya kisiasa ya ulimwengu imetengeneza vikwazo kwa ushiriki kamili wa baadhi ya makundi ya watu katika kazi ya Hoja. Chuki za kidini na za kitamaduni ambazo wakati fulani zilionekana kupungua zimeibuka upya kwa ukali. Wabahá′i wamejitahidi kushughulikia changamoto hizi kwa ustahimilivu na utulivu. Bado, katika karne iliyopita, hakuna mwitikio bora zaidi kwa nguvu za uadui, zilizoachiliwa ili kupinga maendeleo ya Hoja, ambao umeshuhudiwa kuliko ule wa Wabahá′i wa Iran.

Tangu miaka ya mwanzoni kabisa ya utumishi wa Mlinzi, mateso ambayo Wabahá′i wa Iran walikuwa wameyastahimili katika Zama nzima za Kishujaa yaliendelea na mawimbi ya ukandamizaji mkali yakipita juu ya jumuiya hiyo, yakiongezeka katika ukali wa mashambulio na kampeni iliyopangiliwa vyema ya ukandamizaji iliyofuatia baada ya mapinduzi ya Iran, na ambayo yanaendelea bila kukoma hadi siku ya leo. Licha ya yote waliyoyastahimili, Wabahá′i wa Iran waliitikia kwa ujasiri thabiti na unyumbulikaji chanya. Wameshinda heshima isiyokwisha kupitia mafanikio kama vile uanzishwaji wa Taasisi ya Kibahá′i kwa ajili ya Elimu ya Juu ili kuhakikisha elimu kwa vizazi vinavyofuata, jitihada zao za kubadilisha mitazamo ya raia wenzao wenye fikra zisizo na upendeleo—wawe ndani au nje ya nchi—na zaidi ya yote, ustahimilivu wao wa ukosefu usiohesabika wa haki, ufidhuli, na ufukara ili kuwalinda waumini wenzao, kudumisha uadilifu wa

Imani ya Baháʼuʼlláh katika nchi Yake pendwa, na kulinda uwepo wake kwenye nchi hiyo kama manufaa kwa raia wake. Katika kujionyesha huku kwa sifa ya ujasiri thabiti, ya ibada iliyowekwa wakfu, na kusaidiana, kuna masomo muhimu ya jinsi ambavyo ulimwengu wa Kibaháʼi lazima uitikie kwa ajili ya uchapuzaji wa nguvu za uharibifu ambazo zaweza kutarajiwa katika miaka ijayo.

Kwenye kiini chake, changamoto iliyowasilishwa na mwingiliano wa michakato ya uunganishaji na uchangukaji ni changamoto ya kushikilia kwa uthabiti kwenye maelezo ya Baháʼuʼlláh juu ya uhalisia na kwa mafundisho Yake, ambapo kupinga mvuto wa mijadala yenye utata na iletayo mgawanyiko na maagizo ya kilaghai ambayo huakisi jaribio lisilo na manufaa kuelezea utambulisho wa binadamu na uhalisia wa kijamii kupitia dhana finyu za kibinadamu, falsafa za kiyakinifu, na matamanio yashindanayo. "Tabibu Ajuaye-Yote ameweka kidole Chake juu ya pigo la moyo wa wanadamu. Yeye hubaini ugonjwa na kuamuru tiba, katika hekima Yake isiyokosea", Baháʼuʼlláh husema. "Tunaweza kutambua vyema jinsi mbari nzima ya binadamu ilivyozingirwa na mateso makubwa na yasiyohesabika." Bado, Yeye anaongeza, "Wale ambao wanaleweshwa na kiburi cha ubinafsi wamejiingiza wenyewe kati yake na Tabibu Asiyekosea. Shuhudieni jinsi ambavyo wamewazongomeza watu wote, pamoja na wao wenyewe, katika wavu wa hila zao. Ikiwa Wabaháʼi huzongomezwa katika dhana danganyifu za watu wanaogombana, ikiwa wanaiga tunu, mitazamo na mazoea yanayobainisha zama za kujishughulisha na ubinafsi na kujipendelea mwenyewe kuliko wengine, uachiliaji wa zile nguvu za lazima kwa ajili ya kuwakomboa jamii ya wanadamu kutokana na hali yake mbaya utacheleweshwa na kuzuiliwa. Badala yake! Kama Mlinzi anavyoeleza, "Wajenzi bingwa wa utaratibu wa Ulimwengu unaoinukia wa Baháʼuʼlláh, lazima waparamie vilele bora vya ushujaa kadiri wanadamu wanavyotumbukia katika vilindi vikubwa zaidi vya kukata tamaa, udhalilishaji, mfarakano na dhiki. Waache wasonge mbele hadi kwenye siku zijazo wakiwa wenye kujiamini kwa utulivu kwamba saa ya juhudi zao zenye nguvu kabisa na fursa kuu kwa matendo yao makuu kabisa ya ushujaa lazima ziendane na msukosuko wenye majanga unaoashiria hali duni kabisa katika usitawi unaopungua kwa kasi wa wanadamu."

Hakuna awezaye kutazamia kwa usahihi njia ambayo nguvu za uchangukaji zinakusudiwa kuchukua, machafuko makali jinsi gani yataendelea kuwashambulia wanadamu katika zama hizi za uchungu, au ni vikwazo na fursa gani zinaweza kutokea, hadi mchakato unafikia kilele chake kwenye utokeaji wa ile amani kuu ambayo itaashiria ujio wa hatua ambapo, yakitambua umoja na ujumla wa jamii ya binadamu, mataifa "yatatupilia mbali silaha za kivita na kugeukia kwenye zana za ujenzi upya wa ulimwengu". Jambo moja hata hivyo, la hakika ni: Mchakato wa uunganishaji pia utachapuzwa, ukifuma pamoja daima kwa ukaribu zaidi jitihada za wale wanaojifunza kutafsiri mafundisho ya Baháʼuʼlláh katika uhalisia pamoja na wale walio katika jamii pana wanaotafuta haki na amani. Katika Ujio wa Haki Takatifu, Shoghi Effendi aliwaelezea Wabaháʼi wa Amerika kwamba, kwa kuzingatia ukubwa wenye mipaka wa jumuiya yao na ushawishi mdogo iliokuwa nao, lazima wamakinikie, wakati huo, kwenye ukuaji na maendeleo yake yenyewe kwani ilijifunza kuyatumia Mafundisho. Yeye aliahidi, hata hivyo, kwamba wakati ungefika ambapo wangeombwa kuwashirikisha raia wenzao katika mchakato wa kufanya kazi kwa ajili ya uponyaji na uboreshaji wa taifa lao. Wakati huo sasa umefika. Na umefika sio tu kwa Wabaháʼi wa Amerikai, bali kwa Wabaha'i wa Ulimwengu, kwani nguvu isiyodhihirika ya ujengaji jamii iliyomo katika Imani inaachiliwa kwa viwango vikubwa daima.

Uachiliaji wa nguvu kama hii una athari kwa miongo ijayo. Kila aina ya watu na kila taifa lina jukumu la kutimiza katika hatua inayofuata katika ujenzi mpya wa kimsingi wa jamii ya binadamu. Wote wana umaizi wa kipekee na tajiriba kuchangia kwenye ujenzi wa ulimwengu uliounganika. Na ni jukumu la marafiki, kama wachukuzi wa ujumbe wenye tiba wa Baháʼuʼlláh, kuzisaidia jamii za watu kuachilia uwezo wao uliofichika kufanikisha matamanio yao ya juu kabisa. Katika jitihada hii, marafiki wanashiriki ujumbe huu wenye thamani sana na wengine, wakikazana kuonesha ufanisi wa tiba takatifu kwenye maisha ya watu binafsi na jumuiya, na kufanya kazi pamoja na wale wote wanaothamini na kushiriki tunu na matamanio yale yale. Wakati wafanyavyo hivyo, muono wa Baháʼuʼlláh wa ulimwengu uliounganika utatoa mwelekeo wenye matumaini na dhahiri kwa watu ambao mtazamo wao umepotoshwa kwa mkanganyiko unaoenea ulimwenguni, na njia nzuri kwa ajili ya ushirikiano katika utafutaji wa suluhu ya maradhi ya kijamii yaliyodumu muda mrefu. Kadiri roho ya Imani inavyozidi kupenyeza katika mioyo kwa kuwasha upendo na kuimarisha utambulisho wa pamoja wa wanadamu kama watu wamoja, inaingiza hisia ya utiifu na majukumu makinifu ya kiraia na, badala ya kufuatilia mamlaka ya kidunia, inaelekeza tena nguvu kuelekea kwenye huduma ya haki katika kufuatilia manufaa ya pamoja. Watu wanazidi kutwaa mbinu ya ushauriano, utendaji na tafakari ili kuondoa ushindani na ugomvi usiokoma. Watu binafsi, jumuiya na asasi katika jamii mbalimbali wanazidi kupatanisha jitihada zao, katika kusudi la pamoja, ili kuushinda ushindani wa kimadhehebu, na sifa za kiroho na za kimaadili, ambazo ni msingi kwa maendeleo na usitawi wa mwanadamu, zinajikita mizizi katika tabia za binadamu na desturi za kijamii.

Ulimwengu, kwa ukweli, unajongea kuelekea kwenye hatima yake. Kadiri Hoja ya Baháʼuʼlláh inavyosonga mbele kwenye karne ya pili ya Zama za Ujenzi, acha wote wahamasike na maneno ya mpendwa Mlinzi, ambaye mkono wake uongozao ulibumba isivyobadilika, karne iliyopita. Akiandika mnano 1938 kuhusu utekelezaji wa hatua ya kwanza ya Mpango Mtakatifu, yeye alisema: "Uwezo usio dhahiri ambao kwao Mjalia mwenye uwezo wote ameujalia, bila shaka, utawawezesha wakuzaji wake kutimiza kusudi lao. Mengi, walakini, yatategemea juu ya roho na namna ambayo kazi hiyo itakavyotekelezwa. Kupitia uwazi na uthabiti wa muono wao, kupitia uhai safi wa imani yao, kupitia uadilifu wa tabia zao, kupitia nguvu isiyonyumbulika ya azma lao, ubora usiofananishwa wa shabaha na makusudi yao, upeo usiozidiwa wa mafaniko yao, wale wanaofanya kazi kwa ajili ya utukufu wa Jina Kuu Kabisa ... wanaweza kuonesha vizuri zaidi kwa jamii isiyoweza kuona mbali, isiyo na imani, na isiyotulia wanayotoka nguvu zao kutoa kimbilio la usalama kwa ajili ya wana-jamii kwenye saa ya utambuzi wa maangamizi yao. Ni hapo na ni hapo tu ndipo mti huu mchanga, uliopachikwa kwenye udongo wenye rutuba wa Utaratibu wa Kiutawala ulioteuliwa Kitakatifu, na kutiwa nguvu kwa michakato yenye nguvu ya asasi zake, utakapozaa matunda yake bora na yaliyokusudiwa.”

Nyumba ya Haki ya Ulimwengu